BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# RIPOTI YA KAMATI YA BAJETI YA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

FEBUARI, 2022

# YALIYOMO


*SEHEMU YA KWANZA* ........ *5*

UTANGULIZI ........ 5

Muundo wa Kamati ........ 5

*SEHEMU YA PILI* ........ *7*

TATHMINI YA MWENENDO WA UKUAJI WA HALI YA UCHUMI ........ 7

*SEHEMU YA TATU* ........ *11*

TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2020/2021 NA NUSU MWAKA (JULAI – DISEMBA 2021/2022) ........ 11

Deni la Taifa ........ 12

Uimarishaji wa Mifumo ya Ukusanyaji wa Mapato ........ 12

Maoni na Ushauri wa Kamati ........ 13

*SEHEMU YA NNE* ........ *14*

UCHAMBUZI WA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA TAASISI NA MASHIRIKA YA UMMA 14

SHIRIKA LA MELI ZANZIBAR (SHIPCO) ........ 14

WAKALA WA SERIKALI MTANDAO ZANZIBAR (eGAZ) ........ 15

Ziara ya Kamati ya Bajeti kwa Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA) – Dar es Salaam 17

BODI YA MIKOPO YA ELIMU YA JUU ZANZIBAR (BMEJZ) ........ 18

WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI ........ 21

SHIRIKA LA BANDARI LA ZANZIBAR ........ 24

MAMLAKA YA UDHIBITI WA UTAFUTAJI NA UCHIMBAJI WA MAFUTA NA GESI ASILIA ZANZIBAR ( ZPRA) ........ 26

KITENGO CHA MADENI CHA AFISI YA RAIS FEDHA NA MIPANGO ........ 27

BODI YA MAPATO ZANZIBAR (ZRB) ........ 28

MAMLAKA YA VIWANJA VYA NDEGE ZANZIBAR (ZAA) ........ 30

SHIRIKA LA BIASHARA LA TAIFA ZANZIBAR (ZSTC) ........ 31

WIZARA YA AFYA, USTAWI WA JAMII, WAZEE, JINSIA NA WATOTO ........ 33

WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA UCHUKUZI ........ 34

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA - TAWI LA ZANZIBAR ........ 35

WAKALA WA MAENDELEO YA VIWANDA VIDOGO VIDOGO NA VYA KATI (SMIDA) ........ 37

*SEHEMU YA TANO* ........ *40*

UCHAMBUZI WA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU NA BAJETI YA MAMLAKA YA SERIKALI ZA MITAA 40

*SEHEMU YA SITA 43*

UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO NA PROGRAMU MBALI MBALI 43

Ushiriki wa Sekta Binafsi katika kufadhili Miradi ya Maendeleo. 43

MIRADI YA MAENDELEO ILIYOFANYIWA KAZI NA KAMATI YA BAJETI 44

MRADI WA ELIMU YA LAZIMA KUPITIA MRADI MDOGO WA KUIMARISHA ELIMU YA SEKONDARI (ZANZIBAR IMPROVING STUDENT PROSPECTS - ZISP) 44

MRADI WA UKUZAJI UCHUMI JUMUISHI ZANZIBAR (BOOSTING INCLUSIVE GROWTH FOR ZANZIBAR-BIG Z) 44

MRADI WA UIMARISHAJI WA UTALII KWA WOTE 45

MRADI WA UHUISHAJI NA UIMARISHAJI WA MFUMO WA USAMBAZAJI MAJI ZANZIBAR (INDIA) 47

MRADI WA UCHIMBAJI WA VISIMA ZANZIBAR - RAS EL KHAIMAH 48

MRADI WA UIMARISHAJI WA MAENEO YA VIWANDA (INDUSTRIAL PARK) - UNGUJA NA PEMBA 49

MRADI WA USAFISHAJI WA MAJI TAKA KATIKA ENEO LA MSINGINI CHAKE CHAKE - PEMBA 52

PROGRAMU YA KUIMARISHA MIUNDOMBINU YA ELIMU NA MRADI WA KUIMARISHA ELIMU MBADALA NA MAFUNZO YA AMALI 53

MRADI WA UJENZI WA MIUNDOMBINU YA UMWAGILIAJI MAJI ZANZIBAR 54

MRADI WA KUJENGA UWEZO NA MATENGENEZO YA MIUNDOMBINU YA UMEME ZANZIBAR (CBMP) NA MRADI WA KUIFANYIA MABADILIKO SEKTA YA NISHATI (ZEST) PAMOJA NA KUFANYA ZIARA KATIKA BAADHI MAENEO YA MIRADI HIYO 55

TAARIFA YA UKODISHWAJI WA VISIWA VIDOGO VIDOGO VILIVYOPO UNGUJA NA PEMBA AMBAVYO VINATUMIKA KWA SHUGHULI ZA UTALII 57

MRADI WA MJI SALAMA UNGUJA NA PEMBA 59

MRADI WA VIWANDA VYA USHONI WA NGUO NA VIATU KVZ - MTONI 61

SHIRIKA LA NYUMBA ZANZIBAR 62

Ziara ya Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) Dar es Salaam 64

MRADI WA MFUKO WA MAENDELEO YA JAMII (TASAF III) 64

Ziara ya Kamati katika Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) - Dar Es Salaam 66

MRADI WA UJENZI WA SKULI YA SEKONDARI NA UFUNDI JKU – MTONI 66

MIRADI YA UJENZI WA MAHANGA NA NYUMBA ZA ASKARI WA JKU NA CHUO CHA MAFUNZO 68

MRADI WA UJENZI WA JENGO LA STUDIO NA OFISI ZA SHIRIKA LA UTANGAZAJI ZANZIBAR (ZBC) - PEMBA 68

MRADI WA UJENZI WA BOHARI YA DAWA VITONGOJI - PEMBA 70
MRADI WA UNUNUZI WA MITAMBO YA UCHAPAJI YA WAKALA WA SERIKALI WA UCHAPAJI ZANZIBAR 72
MRADI WA UIMARISHAJI NA UTOAJI WA MATANGAZO YA ZBC 73
PROGRAMU YA MAENDELEO YA MAKAAZI KWA KIPINDI CHA JULAI - SEPTEMBA 2021/2022 74
*SEHEMU YA SABA 76*
HITIMISHO 76

# SEHEMU YA KWANZA

## UTANGULIZI

Kwanza kabisa, naomba nianze kwa kumshukuru Allah (S.W) kwa kutujaalia uzima na afya njema tukaweza kutekeleza majukumu yetu kama tulivyojipangia katika kuwatumikia wananchi wa Zanzibar.

Kwa mujibu wa Kanuni ya 109 (15) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi (Toleo la 2020) ambayo inaitaka kila Kamati ya Kudumu ya Baraza kuwasilisha ripoti ya shughuli zake mbele ya Baraza katika Mkutano wa mwezi wa Febuari au wakati mwengine ambapo Kamati ya Uongozi na Shughuli za Baraza itaamua.

Kamati ya Bajeti ilitekeleza majukumu yake kama yalivyoanishwa katika Jadweli la Kwanza chini ya Kanuni ya 107(3) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi. Katika kutekeleza majukumu hayo, Kamati ilikutana na Wizara mbali mbali, Taasisi, Mamlaka, Mashirika, Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na wadau mbalimbali kwa ajili ya kupokea taarifa za utendaji kazi na kupokea maoni mbali mbali. Katika utekelezaji wa majukumu hayo Kamati imetoa maoni na ushauri kwa Serikali na taasisi hizo kwa lengo la kuimarisha utendaji.

## Muundo wa Kamati

Kamati ya Bajeti imeundwa na Wajumbe saba (7), Makatibu Kamati watatu (3) na Msaidizi Mmoja (1) wa Mheshimiwa Mjumbe kama ifuatavyo:

| | |
|---|---|
| 1. Mhe. Ali Suleiman Ameir (Mrembo) | Mwenyekiti |
| 2. Mhe. Anna Athanas Paul | Makamo Mwenyekiti |
| 3. Mhe. Harusi Said Suleiman | Mjumbe |
| 4. Mhe. Issa Haji Ussi Gavu | Mjumbe |
| 5. Mhe. Miraji Khamis Mussa | Mjumbe |
| 6. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa | Mjumbe |

7. Mhe. Prof. Omar Fakih Hamad Mjumbe
8. Ndg. Asha Said Mohamed Katibu
9. Ndg. Shaib Fadhil Shaib Katibu
10. Ndg. Yussuf Mkamba Mwinyi Katibu
11. Ndg. Yustina Edward Joseph Msaidizi wa Mjumbe

Katika kutekeleza majukumu yake, Kamati ya Bajeti ilijielekeza zaidi katika kufuatilia mwenendo wa ukusanyaji mapato na kusimamia matumizi ya Serikali pamoja na kufanya uchambuzi wa masuala mbalimbali ya ukuaji wa uchumi na utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya Zanzibar.

Taarifa ya Kamati ya Bajeti imegawanyika katika Sehemu Kuu Saba (7). **Sehemu ya Kwanza** ni Utangulizi; **Sehemu ya Pili** ni Tathmini ya Mwenendo wa Ukuaji wa Hali ya Uchumi Zanzibar; **Sehemu ya Tatu** ni Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2020/2021 na Nusu Mwaka wa 2021/2022 (Julai – Disemba 2021/2022); **Sehemu ya Nne** ni Uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti ya Taasisi na Mashirika ya Umma; **Sehemu ya Tano** ni Uchambuzi wa Utekelezaji wa Majukumu na Bajeti ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa; **Sehemu ya Sita** ni Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo; **Sehemu ya Saba** ni Hitimisho.

# SEHEMU YA PILI

## TATHMINI YA MWENENDO WA UKUAJI WA HALI YA UCHUMI

### Mfumko wa Bei

Katika mwaka 2021, Mfumko wa Bei ulipungua na kufikia wastani wa asilimia 1.7 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 3.4 kwa mwaka 2020. Mfumko wa Bei umeendelea kupungua na kubaki katika kiwango cha tarakimu moja. Hali hii inasaidia kuendelea kuwepo kwa utulivu wa bei za bidhaa na huduma.

Jadweli Nam. 1: Mfumko wa Bei kwa kila mwezi kwa mwaka 2020 na 2021

| Mwezi | Mfumko wa Bei | |
|---|---|---|
| | 2020 | 2021 |
| Januari | 4.9 | 0.5 |
| Februari | 6.2 | 0.7 |
| Machi | 5.0 | 1.5 |
| Aprili | 4.7 | 1.9 |
| Mei | 5.3 | 0.8 |
| Juni | 3.4 | 1.9 |
| Julai | 3.6 | 2.2 |
| Agosti | 2.4 | 2.1 |
| Septemba | 2.1 | 2.4 |
| Oktoba | 1.6 | 2.1 |
| Novemba | 1.0 | 2.2 |
| Disemba | 0.5 | 2.4 |
| Wastani kwa Mwaka | 3.4 | 1.7 |

Chanzo: Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali

Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hii sambamba na kuishauri kuendelea na

udhibiti wa bei ya mafuta kulingana na bei ya soko la dunia, ihakikishe upatikanaji wa chakula cha kutosha katika masoko yetu pamoja na kuongeza juhudi za kuuza bidhaa zetu nje ya nchi ili kuwe na akiba ya kutosha ya fedha za kigeni ili kuendelea kuudhibiti mfumko wa bei.

## Mwenendo wa Sarafu ya Tanzania

Thamani ya Shilingi ya Tanzania imeendelea kuwa tulivu ikilinganishwa na sarafu nyengine duniani na nchi washirika wa biashara. Katika kipindi cha Disemba 2021, dola moja ya Marekani ilibadilishwa kwa wastani wa TZS 2309.24, ikilinganishwa na wastani wa TZS 2,309.99 katika kipindi kama hicho mwaka 2020.

Aidha, Shilingi ya Tanzania ilibadilishwa kwa wastani wa TZS 20.39 kwa Shilingi moja ya Kenya katika kipindi cha Disemba mwaka 2021 ikilinganishwa na wastani wa TZS 21.14 kwa shilingi moja ya Kenya katika kipindi kama hicho mwaka 2020. Kadhalika, katika kipindi hicho cha Disemba 2021, Shilingi ya Tanzania ilibadilishwa kwa wastani wa TZS 0.65 kwa shilingi moja ya Uganda ikilinganishwa na wastani wa TZS 0.63 katika kipindi kama hicho mwaka 2020. (Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania)

Utulivu wa Sarafu ya Tanzania unatokana na kuwepo kwa mfumko wa bei wa chini ambao unaendana na vigezo na matakwa ya jumuiya ya Afrika Mashariki pamoja na kuwepo kwa sera bora za fedha na uchumi Tanzania.

## Idadi ya Watalii

Jumla ya watalii waliongia nchini kwa mwaka 2021 imefikia 394,185 kutoka jumla ya watalii 260,644 waliongia katika mwaka 2020. Kuongezeka kwa idadi ya watalii katika mwaka 2021 imechangiwa zaidi na kuwepo kwa chanjo ya UVIKO 19, ambayo imepelekea baadhi ya nchi kuondosha vikwazo vya kusafiri katika nchi zao hususan Bara la Ulaya na Asia kutokana na kupungua maambukizi kwa kiwango kikubwa duniani hali ambayo imepelekea kuanza kuimarika kwa sekta

mbali mbali za kiuchumi ikiwemo sekta ya utalii ambayo inachukuwa asilimia kubwa ya uchumi wa nchi yetu.

Jadweli Nam. 2: Idadi ya Watalii kwa kila mwezi kwa mwaka 2020 na 2021

| Mwezi | Idadi ya Watalii | |
|---|---|---|
| | 2020 | 2021 |
| Januari | 61,461 | 49,868 |
| Februari | 61,752 | 51,574 |
| Machi | 33,801 | 43,821 |
| Aprili | 334 | 13,839 |
| Mei | 197 | 9,280 |
| Juni | 353 | 20,416 |
| Julai | 3,079 | 29,714 |
| Agosti | 4,366 | 34,425 |
| Septemba | 5,422 | 25,817 |
| Oktoba | 12,157 | 31,826 |
| Novemba | 29,128 | 35,438 |
| Disemba | 48,594 | 48,167 |
| Jumla | 260,644 | 394,185 |

Chanzo: Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali

Kufahamu takwimu za ongezeko la watalii pekee bila ya kufahamu takwimu za mapato yanayotokana na idadi hiyo kubwa ya watalii haitoshi kujua mafanikio ya sekta ya utalii. Kujua takwimu za mapato itatusaidia kupima mapato ya nchi kama yanaongezeka sambamba na kuongezeka kwa idadi ya watalii. Kuongezeka kwa mapato yanayotokana na watalii haitegemei kigezo cha kuongezeka kwa idadi ya watalii pekee bali pia aina ya watalii wanaokuja, siku watakazokaa nchini (length of stay) nakadhalika.

Ni wazi kwamba, sekta ya utalii ni miongoni mwa sekta zinazokuwa kwa kasi sana Zanzibar na ina mchango mkubwa sana katika uchumi wa nchi yetu. Hata hivyo, bado kuna changamoto za msingi ambazo zinapaswa kufanyiwa kazi kwa haraka ili sekta hii kuwa na mafanikio. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali, kutengeneza mfumo utakaowezesha kujua mapato yote yanayotokana na sekta ya utalii tokea mgeni anapowasili mpaka atakapoondoka.

Maoni na Ushauri wa Jumla wa Kamati

i. Licha ya kwamba Tathmini ya Mwenendo wa Hali ya Uchumi inaonesha kuendelea kuimarika kwa hali ya uchumi Zanzibar, kwa ujumla bado kuna changamoto kubwa ya kuhakikisha kuwa ukuaji huu unaenda sambamba na upunguzaji wa umaskini hasa kwa kuziwezesha sekta za uvuvi, kilimo na ujasiriamali. Sekta hizi ndio sekta ambazo zinazohusisha idadi kubwa ya wananchi. Kamati inasisitiza umuhimu wa kuzingatia ukuaji wa uchumi unaogusa sekta zinazoajiri wananchi wengi ili kupunguza umaskini.

ii. Takwimu za mwenendo wa hali ya uchumi zinaonesha mafanikio katika sekta mbali mbali za kiuchumi lakini bado kumekuwa na malalamiko ya hali za kimaisha za wananchi wengi. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba takwimu zinazokusanywa na kufanyiwa uchambuzi zina uhalisia na zinaakisi hali halisi.

# SEHEMU YA TATU

## TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2020/2021 NA NUSU MWAKA (JULAI – DISEMBA 2021/2022)

### Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka 2020/2021

Takwimu zinaonesha kwamba, hadi kufikia Juni, 2021, mapato ya Serikali yalifikia TZS 940.2 bilioni sawa na asilimia 59.5 ya lengo la kukusanya TZS 1,579.2 bilioni. Matumizi ya kazi za kawaida yalikuwa TZS 740.1 bilioni ambayo sawa na asilimia 77.6 na matumizi ya kazi za maendeleo yalikuwa TZS 213.7 bilioni sawa na asilimia 22.4 ya kiasi kilichopangwa kutumika.

Pamoja na jitihada za Serikali katika kuongeza makusanyo ya mapato, bado kiwango hiki cha makusanyo si cha kuridhisha ukilinganisha na mahitaji makubwa ya fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida pamoja na utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Ni vyema Serikali ikafanya jitihada ya kutafuta maeneo mengine ya vyanzo vya mapato (potential areas) sambamba na kukusanya kwa ufanisi ili iweze kugharamia bajeti yake iliyopangwa na hivyo kukidhi mahitaji halisi ya wananchi. Takwimu zinaonesha zaidi ya asilimia 77 ya mapato yametumika zaidi katika kugharamia kazi za kawaida na chini ya asilimia 23 ndio zilitumika kwa ajili kazi za maendeleo. Kwa mwenendo huu, inamaanisha kwamba maendeleo yetu yanakuwa kwa kasi ndogo sana.

### Mwenendo wa Mapato na Matumizi kwa Nusu Mwaka wa 2021/2022 (Julai – Disemba 2021/2022)

Kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali imekadiria kukusanya mapato na kufanya matumizi ya jumla ya TZS 1,845.6 bilioni zikijumuisha TZS 1,829.9 bilioni kwa Serikali Kuu na TZS 15.7 bilioni kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa. Matumizi ya kazi za kawaida yalikadiriwa kuwa TZS 947.2 bilioni sawa na asilimia 51.8 na

kwa kazi za maendeleo jumla ya TZS 882.8 bilioni sawa na asilimia 48.2.

Kwa kipindi cha nusu mwaka 2021/2022 (Julai – Disemba 2021), Serikali imefanikiwa kukusanya TZS 466.5 bilioni sawa na asilimia 69.3 ya makadirio ya TZS 672.8 bilioni kwa kipindi hicho, na asilimia 25.3 ya makadirio ya TZS 1,845.6 bilioni kwa mwaka mzima wa 2021/2022. Matumizi halisi ni TZS 367.9 bilioni kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 79, na kwa upande wa matumizi ya kazi za maendeleo zimetumika TZS 97.6 bilioni ambazo ni sawa na asilimia 21 ya jumla kilichokusanywa.

Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kipindi cha nusu mwaka 2021/2022 yamefikia Jumla ya TZS 4.8 bilioni kutokana na vyanzo vyake vya ndani, makusanyo hayo sawa na asilimia 78.7 ya makadirio ya kukusanya TZS 6.1 bilioni kwa kipindi hicho na ni sawa na asilimia 30.6 ya makadirio ya mwaka nzima ya TZS 15.7 bilioni. Hali hii ya ukusanyaji wa mapato hairidhishi, ni vyema Serikali ikapanga makadirio yenye uhalisia kulingana na uwezo wetu wa ukusanyaji mapato badala ya kuweka malengo makubwa ambayo hatuwezi kuyafikia.

## Deni la Taifa

Hadi kufikia Disemba 2021, Deni la Taifa limefikia TZS 1,127.5 bilioni ikilinganishwa na TZS 896.6 bilioni Disemba 2020. Hii inamaanisha kwamba, kwa kipindi cha mwaka mmoja Deni la Taifa limeongezeka kwa TZS 230.9 bilioni sawa na ongezeko la asilimia 25.6.

Pamoja na kuwa deni hili ni himilivu kwa vigezo vyote bado limekuwa ni mzigo mkubwa kwa nchi yetu. Deni hili limeendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka kutokana na kuendelea kukopa sambamba na kuongezeka kwa gharama za kuhudumia deni. Kamati inaishauri Serikali, kukopa mikopo yenye masharti nafuu sambamba na kuzielekeza fedha za mikopo katika miradi itakayochochea ukuaji wa uchumi.

## Uimarishaji wa Mifumo ya Ukusanyaji wa Mapato

Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanzisha mfumo wa kukusanya mapato ya Serikali kwa njia ya kielektroniki ujulikanao kama ZanMalipo. Hatua hii itasaidia kudhibiti mianya ya upotevu wa fedha pamoja na kupunguza urasimu katika ulipaji wa fedha (Kodi, ada na tozo). Pia, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanza rasmi matumizi ya Mashine za Kielektroniki za Utoaji wa Risiti (VFD's). Kamati inasisitiza kwamba, changamoto mbali mbali ambazo zimejitokeza katika kutumia mifumo hiyo ili iwe endelevu naiweze kufanya kazi kwa ufanisi mkubwa.

## Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kumekuwepo na ucheleweshaji mkubwa wa fedha za miradi ya maendeleo kiasi ambacho ufanisi unakosekana katika utekelezaji wake na gharama inaongezeka. Kamati inashauri, ni bora tupange miradi michache lakini tutakayoweza kuitekeleza ili kumaliza kwa wakati na kuanza kutoa tija sambamba na kuepuka kuongezeka kwa gharama kunakosababishwa na kuchelewa kumalizika kwa mradi husika.

ii. Kamati inaishauri Serikali kuongeza umakini katika usimamizi wa madeni sambamba na kuhakikisha miradi yote inayotekelezwa kwa fedha za mikopo inamalizika kwa wakati na inatoa tija. Kufanya hivyo, kutapunguza mzigo wa madeni, kutaongeza mapato na huduma ambazo zitasaidia katika ukuaji wa uchumi wa nchi yetu.

iii. Makadirio ya matumizi ya Serikali yanaonesha kwamba, fedha nyingi zinatumika katika matumizi ya kawaida ukilinganisha na fedha zinazotumika katika kazi maendeleo, hali hii inapelekea kasi ndogo ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo hasa ikizingatiwa kwamba upatikanaji wa fedha kidogo zinazotengwa kwa ajili ya maendeleo si wa uhakika.

iv. Kamati inaishauri Serikali kuanzisha chombo maalum ambacho kitahusika na kutambua vyanzo vyote vya mapato na kuweka makisio ya mapato kwa kila mwaka kwa taasisi zote za Serikali na Mashirika ya Umma. Hii ni

kutokana na kila taasisi au Shirika kujipangia makisio ya mapato yake wenyewe. Hali hii husababishwa taasisi au Shirika kuweka makisio madogo ya kukusanya mapato ili kuonekana zimevuka lengo la makusanyo.

# SEHEMU YA NNE

## UCHAMBUZI WA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA TAASISI NA MASHIRIKA YA UMMA

Kwa madhumuni ya kuhakikisha kunakuwepo utekelezaji bora wa bajeti za Taasisi za Serikali na Mashirika ya Umma ili kufikia lengo la ukusanyaji mapato na matumizi kwa ufanisi na pia kuweza kutoa gawio kwa Serikali. Kamati ya Bajeti ilipitia na kujadili taarifa za utekelezaji wa bajeti za Taasisi za Serikali na Mashirika ya Umma kama yanavyoonekana katika ripoti hii.

## SHIRIKA LA MELI ZANZIBAR (SHIPCO)

Kutokana na nchi yetu kuwa ni nchi ya visiwa, kuimarisha sekta ya usafiri baharini ni jambo muhimu kwa lengo la kurahisisha usafiri kutakakopelekea kuchochea kwa kiasi kikubwa ukuaji wa uchumi wa nchi yetu sambamba na ustawi wa wananchi kwa ujumla. Kwa kuliona hilo, Serikali ilianzisha Shirika la Meli Zanzibar mwaka 1976.

Shirika la Meli Zanzibar limepewa jukumu la kuzisimamia na kuziendesha meli zote za Serikali pamoja na kutoa huduma za uwakala kwa meli za kigeni zinazoingia katika bandari za Zanzibar.

Licha ya umuhimu mkubwa wa Shirika la Meli Zanzibar, bado Shirika limekuwa likizorota katika utekelezaji wa kazi zake. Tokea Shirika lilipoanzishwa hadi hii leo, ilitakikana liwe linajiendesha kwa ufanisi tofauti na ilivyo sasa ambapo Shirika linasuasua sana. Kumekuwepo na hatua mbali mbali za kulinisuru Shirika kama vile, kufanywa mabadiliko kadhaa ya kisheria ili Shirika liweze kujiendesha

kibiashara na kutoa huduma bora kwa wananchi lakini bado limekuwa likipata hasara.

### Changamoto za Shirika la Meli Zanzibar

Miongoni mwa changamoto za msingi za Shirika la Meli Zanzibar ni kama zifuatazo:

i. Shirika kukabiliwa na madeni makubwa.
ii. Shirika kutokuwa na meli za abiria na mizigo.
iii. Shirika kukabiliwa na uhaba wa mabaharia wenye weledi (competence).
iv. Kutokuwepo kwa mfumo wa mishahara ya ubaharia na kutotambulika katika taasisi za kiutumishi za Serikali.

### Maoni na Ushauri wa Kamati

Ili lengo la Shirika la kuweza kujiendesha kibiashara na kutoa huduma kwa jamii lifikiwe, Kamati ya Bajeti inashauri mambo yafuatayo:

i. Serikali inapaswa kuweka mipango na mikakati madhubuti inayotekelezeka ili kulinusuru Shirika, kwani hali ilivyo sasa Shirika linaelekea kufa au kubaki kuwa wakala tu kwa meli za kigeni.
ii. Serikali ifanye utafiti wa namna ya kuliwezesha Shirika kujiendesha kwa faida.
iii. Serikali inunue meli mpya ambazo zitaweza kufanya kazi kwa ufanisi katika mazingira yetu. Kitu kikubwa cha kukizingatia ni kuhakikisha gharama za uendeshaji meli hizo hazizidi mapato yake.
iv. Serikali iangalie muundo wa utumishi wa mabaharia ili kuleta ufanisi katika kazi. Jambo hili litasaidia wafanyakazi kutokimbia na kwenda katika kampuni za binafsi.
v. Serikali iweke mkakati na mpango wa namna ya kuyalipa na kuyadhibiti madeni ya Shirika la Meli Zanzibar.
vi. Serikali iharakishe uuzwaji wa meli ya MV Mapinduzi II, kwani kuchelewa kufanya hivyo kunaliongezea gharama Shirika.

vii. Shirika lijipange upya katika kufanya shughuli za uwakala hususani katika uajiri wa wafanyakazi wapya wenye weledi na matumizi ya teknolojia. Kwa sasa uwakala ndio unaoingiza mapato kwa Shirika.

## WAKALA WA SERIKALI MTANDAO ZANZIBAR (eGAZ)

Serikali Mtandao ni matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika utendaji kazi Serikalini na utoaji wa huduma kwa umma. Madhumuni ya kuanzishwa kwa Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar (eGAZ) ni kuimarisha utendaji kazi na utoaji huduma za Serikali kwa kutumia TEHAMA. Matumizi ya TEHAMA yanasaidia kurahisisha mawasiliano baina ya taasisi mbali mbali za Serikali pamoja kupunguza gharama za mawasiliano. Kuongeza mapato kwa kuimarisha uwazi na kuzuia uvujaji wa mapato ya Serikali. Jukumu jengine la Wakala, ni kuziunganisha taasisi za umma na mkonga wa taifa.

Serikali Mtandao ina fursa kubwa ya kuleta mabadiliko katika utendaji kazi Serikalini ili kutoa huduma bora kwa wananchi na vile vile kuiwezesha Serikali kuimarisha ukusanyaji na kudhibiti uvujaji wa mapato.

### Changamoto za Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar (eGAZ)

Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar (eGAZ) inakabiliwa na changamoto kadhaa katika kusimamia, kuratibu pamoja na kutekeleza majukumu yake. Miongoni mwa changamoto hizo ni:

i. Wakala inakabiliwa na uhaba wa rasilimali fedha.
ii. Kuchelewa kuidhinishwa muundo wa Wakala, jambo ambalo linapelekea kupunguza ufanisi wa utendaji kazi.
iii. Wakala inakabiliwa na uhaba wa watendaji mahiri kwenye maeneo mbali mbali ya utaalamu katika TEHAMA.
iv. Kuwepo kwa uhaba wa vitendea kazi.
v. Kuwepo kwa ufinyu wa nafasi ya kufanyia kazi. Kwa sasa, Wakala inatumia vyumba viwili tu, hali ambayo inapelekea wafanyakazi kukaa wengi katika

chumba kimoja.

vi. Kutopata ruzuku kutoka Serikalini.

Maoni na Ushauri wa Kamati

Kwa ajili ya kufikiwa lengo na dhamira ya kuanzishwa Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar, Kamati inaishauri Serikali mambo yafuatayo:

i. Serikali iwapatie jengo la Ofisi kwa ajili ya kuimarisha mazingira ya utekelezaji wa majukumu ya Wakala kama taasisi inayojitegemea.
ii. Serikali iiangalie Wakala kwa jicho la upekee kwa kufanya jitihada katika kuwapatia rasilimali fedha za kutosha, vitendea kazi na rasilimali watu ili mafanikio na tija ya kuanzishwa Wakala iweze kufikiwa.
iii. Serikali inapaswa kuipatia Wakala ruzuku. Hii ni kwa mujibu wa Sheria ya Kuanzisha Wakala wa Serikali Mtandao, Kazi zake na Mambo mengine yanayohusiana na hayo, Nam. 12 ya mwaka 2019, Kifungu cha 24 (a).
iv. Kuanzia mwaka ujao wa fedha, Serikali iiruhusu Wakala kuandaa taarifa ya mapato na matumizi yake. Jambo hili ni kwa mujibu wa Sheria ya Kuanzisha Wakala wa Serikali Mtandao, Kazi zake na Mambo mengine yanayohusiana na hayo, Nam. 12 ya mwaka 2019, Kifungu cha 27 (2)
v. Serikali iweke mikakati thabiti ya kuimarisha Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar sambamba na kupewa kazi na taasisi za umma.

## Ziara ya Kamati ya Bajeti kwa Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA) – Dar es Salaam

Kamati ya Bajeti ilifanya ziara Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA) – Dar es Salaam kwa lengo la kujifunza utekelezaji wa Serikali Mtandao ili iweze kuishauri vyema Serikali pamoja na Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar (eGAZ).

Jukumu la msingi la Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA) ni kuratibu, kusimamia na kukuza jitihada za Serikali Mtandao pamoja na kuhimiza uzingatiaji wa Sera, sheria, Kanuni na Miongozo ya Serikali Mtandao katika taasisi za umma, kwa ajili

ya kuhakikisha kuwa taasisi za umma zinatumia TEHAMA kwa usahihi ili kufikia malengo yaliyokusudiwa. Lengo kuu la Serikali Mtandao ni kuongeza tija na ufanisi katika utendaji kazi wa Serikali, ikiwemo kupunguza gharama za utendaji na kuimarisha utoaji wa huduma kwa umma, ili zipatikane kwa urahisi, haraka na kwa gharama nafuu.

Katika ziara hiyo, Kamati ya Bajeti kwa Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA) – Dar es Salaam imejifunza mambo mbali mbali ambayo yanaweza kusaidia katika ufanyaji kazi wa Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar (eGAZ). Miongoni mwa mambo hayo ni kama ifuatavyo:

i. Kuimarisha Utafiti, Ubunifu na Uendelezaji wa Serikali Mtandao kwa kuanzisha Utafiti, Ubunifu na Uendelezaji wa Serikali Mtandao.
ii. Kusimamia, kuendesha na kuendeleza vituo vya Serikali vya kuhifadhia mifumo na taarifa (Data Centers).
iii. Kusanifu, kujenga na kusimamia uendeshaji wa mifumo tumizi ya TEHAMA ya kutolea huduma kwa njia simu za mkononi.
iv. Kukagua, Kupitia, Kutathmini na Kushauri kuhusu hali ya Usalama wa Mifumo na Miundombinu ya TEHAMA kwa taasisi za umma, pamoja na kutambua matishio ya kiusalama mitandaoni.
v. Kuipitia, Kuboresha na Kuidhinisha Miradi ya TEHAMA ya taasisi za umma kwa kuzingatia taratibu zilizowekwa.
vi. Kutoa huduma kwa wateja kuhusiana na utekelezaji wa Serikali Mtandao.
vii. Kulea na kutumia vijana wa ndani wenye vipaji na kuwajengea kujiamini katika kutengeneza program zinazofaa kutokana na changamoto zilizopo nchini.

## BODI YA MIKOPO YA ELIMU YA JUU ZANZIBAR (BMEJZ)

Awali Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar (BMEJZ) ilianza kama Mfuko wa Elimu Zanzibar mwaka 2006. Serikali ilianzisha Mfuko wa Elimu kwa ajili ya malipo ya ada ya Masomo na Mitihani kwa wanafunzi wanaosoma elimu ya juu

kwa ngazi tofauti, Cheti, Diploma na Shahada. Wanafunzi na Wazazi wao walitakiwa kukidhi gharama za Chakula na Malazi.

Mwaka 2011, Bodi ilianzishwa kupitia "The Zanzibar Higher Education Loans Board Act, No.3/2011" na ilianza kazi Agosti 2011 kama taasisi inayojitegemea. Bodi imeanzishwa kwa malipo na urejeshaji wa mikopo ya Elimu ya Juu kutoka kwa wanafunzi waliohitimu.

Majukumu makuu ya Bodi ni pamoja na:

i. Kutoa mikopo kwa wanafunzi wenye uhitaji ambao wanapata nafasi ya kujiunga katika taasisi za elimu ya juu zilizoidhinishwa, lakini hawana uwezo wa kiuchumi wa kulipia gharama za elimu yao.
ii. Kukusanya mikopo inayodaiwa kutoka kwa wanufaika na kuitumia kuendeleza shughuli za Bodi hususan kuwakopesha wanafunzi wengine wenye uhitaji.

Katika mwaka wa fedha 2020/2021, Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar (BMEJZ) ilijiwekea malengo makuu matano yafuatayo: -

i. Kutoa Mikopo kwa wanafunzi 4917 wahitaji wenye sifa za kujiunga na masomo ya elimu ya juu ikiwa wapya 1,900 na wanaoendelea 3,017 katika vyuo vya ndani na nje ya Tanzania.
ii. Kuwapatia ufadhili wa masomo wa SMZ wahitimu 165 wa Kidato cha Sita wenye ufaulu mzuri zaidi wa Daraja la Kwanza ikiwa wapya 60 na 105 wanaoendelea na masomo.
iii. Kusimamia na kufuatilia nafasi 125 za ufadhili wa masomo kutoka kwa washirika wa maendeleo wa nje na ndani ya Tanzania.
iv. Kukusanya kiasi cha TZS 3.51 bilioni kutoka katika vyanzo vya ndani vya BMEJZ, ikiwa marejesho ya mkopo kutoka kwa wanufaika ni 3.09 bilioni, gawio kutoka uwekezaji PBZ TZS 250 milioni na TZS 165 kutoka vyanzo venginevyo.
v. Kuimarisha ufanisi wa utendaji kazi na utoaji huduma.

Jumla ya TZS 16.65 bilioni zilipangwa kutumika kwa mwaka 2020/2021 na TZS 12.76 bilioni ndio yalikuwa matumizi halisi sawa na asilimia 76.64 ya kiasi kilichopangwa. Aidha, kwa upande wa mapato kiasi kilichopangwa kupatikana ni TZS 15.08 bilioni na TZS 8.95 bilioni sawa na asilimia 59.35 ya kiasi kilichopangwa. Asilimia ndogo ya mapato haya, yamechangiwa kwa kiasi kikubwa na kiwango kidogo cha Ruzuku kutoka SMZ kilichopatikana. TZS 11.57 bilioni ya Ruzuku kutoka SMZ ndio zilizokadiriwa kupatikana lakini ni TZS 4.82 bilioni tu ndizo zilizopatikana.

Kwa upande wa mwaka 2021/2022, Bodi ya Mikopo Elimu ya Juu (BMEJZ) ilijiwekea malengo makuu matano yafuatayo:

i. Kutoa Mikopo kwa wanafunzi 4,237 wahitaji wenye sifa za kujiunga na masomo ya elimu ya juu ikiwa wapya 1,104 na wanaoendelea 3,133 katika vyuo vya ndani na nje ya Tanzania.

ii. Kuwapatia ufadhili wa masomo wa SMZ wahitimu 225 wa Kidato cha Sita wenye ufaulu mzuri zaidi wa Daraja la Kwanza ikiwa wapya 40 na 185 wanaoendelea na masomo.

iii. Kusimamia na kufuatilia nafasi 150 za ufadhili wa masomo kutoka kwa washirika wa maendeleo wa nje na ndani ya Tanzania.

iv. kukusanya kiasi cha TZS 4.23 bilioni kutoka katika vyanzo vya ndani vya BMEJZ.

v. Kuimarisha ufanisi wa utendaji kazi na utoaji huduma.

Katika kipindi cha robo ya kwanza cha mwaka wa fedha 2021/2022, Bodi ilitarajia kupokea jumla ya TZS 2.90 bilioni ya ruzuku kutoka SMZ. Hadi kufikia mwishoni mwa Septemba 2021, ilipokea kiasi cha TZS 1.09 bilioni sawa na asilimia 37.59 ya fedha iliyopangwa kutumika.

Aidha, katika robo hii jumla ya TZS 2.45 bilioni zimetumika zikiwemo TZS 1.09 bilioni za ruzuku ya bajeti kutoka SMZ na TZS 1.35 bilioni ni mchango wa Bodi

kutoka vyanzo vya ndani.

Changamoto za Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar (BMEJZ)

i. Fedha za kukopesha wanafunzi hazitoshi.
ii. Kuongezeka kwa waombaji wa mikopo wenye sifa
iii. Ufinyu wa nafasi ya kufanyia kazi pamoja na uhaba wa vitendea kazi.

Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Serikali ihakikishe kwamba, bajeti ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar haina nakisi kwa lengo la kuhakikisha wanafunzi wote wahitaji wenye sifa wanapatiwa mikopo ya elimu ya juu ili kujiendeleza kielimu na kuongeza idadi ya wataalamu wazalendo nchini. Ni hasara kwa nchi, mwananchi mwenye uwezo wa kujiendeleza kukosa fursa ya kufanya hivyo.
ii. Serikali itafute ufumbuzi wa kupata jengo kwa ajili ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar sambamba na vitendea kazi vya kutosha.
iii. Watu wenye mahitaji maalumu wapewe kipaumbele katika kupata mikopo ya elimu ya juu.
iv. Bodi ibakishiwe lengo lake kuu la kutoa mikopo, isibebeshwe jukumu la ufadhili. Iwapo itapewa jukumu hilo, ipelekwe bajeti ya ufadhili ili bodi wabaki na jukumu la uratibu tu.
v. Serikali iangalie namna ya kuwakopesha watumishi wa umma kupitia bodi kwa sababu wengi wao wanakosa fursa ya kupata ufadhili wa kimasomo kutoka katika taasisi zao wanazofanyia kazi.
vi. Serikali iipatie Bodi kupeleka mgao wa fedha kutoka Mfuko wa Fedha wa Kimataifa (IMF) kwani wanastahiki kuwa wanufaika.

## WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI

Miongoni mwa malengo ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi ni kujenga uchumi wa kisasa wa Zanzibar kwa kuzingatia matumizi na usimamizi endelevu wa bahari na ukanda wa pwani. Kusimamia, kuratibu na kuimarisha maendeleo

ya Uchumi wa Buluu Zanzibar ikiwemo Uvuvi, Mazao ya Baharini, Kilimo cha Mwani na Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilimia.

Katika kufanya kazi na Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Kamati ya Bajeti ilipokea taarifa tano (5) kama ifuatavyo:

i. Taarifa ya Wizara kuhusu muelekeo na mikakati iliyojiwekea katika kutekeleza dhana ya uchumi wa buluu.

ii. Taarifa juu ya Mikakati iliyojiwekea katika utekelezaji wa Mradi wa Kuandaa Mpango wa Matumizi ya Bahari na Maeneo Yake.

iii. Taarifa ya Mradi wa Usimamizi wa Shughuli za Uvuvi wa Kanda ya Kusini Mashariki mwa Bahari ya Hindi (SWIOFish).

iv. Taarifa Mradi wa Uimarishaji wa Uvuvi wa Bahari Kuu.

v. Taarifa ya Mashirikiano baina ya SMZ na SMT na Taratibu za Usimamizi wa Uvuvi wa Bahari Kuu (Deep Sea Fishing).

**Taarifa ya Wizara kuhusu muelekeo na mikakati iliyojiwekea katika kutekeleza dhana ya Uchumi wa Buluu**

Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi imeanza utekelezaji wa mikakakti iliyojiwekea katika kutekeleza dhana ya Uchumi wa Buluu yenye kujumuisha matumizi endelevu ya bahari na rasilimali zake pamoja na uhifadhi wa mazingira kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Katika kutekeleza hili, Wizara imefanikiwa kufanya yafuatayo:

i. Kukamilisha mapitio ya Sera ya Uchumi wa Buluu ya mwaka 2020 na kutayarisha Mpango Mkakakti wa Uchumi wa Buluu.
ii. Kuunda, kusajili, kutoa mafunzo na kuvipatia vifaa vikundi vya ushirika kwa wavuvi na wafugaji wa mazao ya baharini
iii. Kutoa uelewa wa dhana ya Uchumi wa Buluu kwa Jamii
iv. Kushajihisha Uwekezaji katika maeneo ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi

Changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji dhana ya Uchumi wa Buluu

i. Kuchelewa kukamilika kwa mchakato wa mapitio ya Sera na Mpango Mkakakti wa Uchumi wa Buluu kwa sababu ya masuala ya taratibu za upatikanaji wa fedha kwa washirika wa maendeleo.
ii. Kuchelewa kuanza kwa Mpango Mkuu wa  Matumizi ya Bahari na Fukwe (Marine Spatial Planning)

Taarifa ya Mradi wa Usimamizi wa Shughuli za Uvuvi wa Kanda ya Kusini Mashariki mwa Bahari ya Hindi (SWIOFISH)

Mradi wa Usimamizi wa Shughuli za Uvuvi wa Kanda ya Kusini Mashariki mwa Bahari ya Hindi (SWIOFish) ni mradi wa miaka sita unaofadhiliwa na Benki ya Dunia (WB). Mradi huu umeanzishwa kwa lengo la kuinua hali za kiuchumi, kijamii na kimazingira kwa jamii zinazoishi katika ukanda wa kusini magharibi mwa bahari ya hindi (SWIO Countries) kutokana na uvuvi endelevu. Mradi wa SWIOFish ulianza rasmi rasmi Juni 2015 na ulitarajiwa kumalizika Septemba 2021 lakini umeongezewa muda hadi Septemba 2022.

Changamoto ya Mradi wa SWIOFish

i. Mripuko wa Ugonjwa wa KORONA umeathiri utekelezaji wa kazi za ushauri elekezi wa uwekaji maboya, uandaaji wa mfumo wa taarifa na uwekaji wa mipaka baharini.

Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Mradi wa SWIOFish umefikia asilimia kubwa ya utekelezaji lakini bado haujaleta tija. Kamati inaishauri Serikali, kuhakikisha miradi inayobuniwa ioneshe mafanikio ya wazi wazi kwa wananchi.

ii. Kamati inashauri kuwepo ushirikishwaji wa wananchi na wanufaika mbali mbali katika utekelezaji wa miradi kwani mara nyingi miradi huwa inajuulikana na wataalamu tu.

## Taarifa ya Mradi wa Uimarishaji wa Uvuvi wa Bahari Kuu

Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi inaendeleza lengo la kuwasaidia kuwasaidia na kuwawezesha wavuvi kuweza kuvua Uvuvi wa Bahari Kuu ili kuongeza kiwango cha uvuvi na tija pamoja na kupunguza mkusanyiko wa wavuvi katika maeneo ya hifadhi.

## Changamoto za Mradi

i. Kuongezeka kwa uvuvi haramu.

ii. Matumizi ya teknolojia duni ya uvuvi

iii. Leseni za uvuvi zinazotolewa Zanzibar kutotambuliwa na kutumika Tanzania Bara.

## Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inaishauri Serikali kuimarisha uwekezaji katika sekta ya uvuvi hususani miundombinu ya uvuvi na kuhakikisha wavuvi wanatoka katika matumizi ya kuvua kwa mazoea na kuelekea katika kutumia teknolojia za kisasa za uvuvi.

ii. Wizara ichukuwe jitihada ya kuwapa elimu wavuvi juu ya athari ya uvuvi haramu katika mazingira na viumbe vilivyomo baharini.

## Taarifa ya Mashirikiano baina ya SMZ na SMT na Taratibu za Usimamizi wa Uvuvi wa Bahari Kuu (Deep Sea Fishing)

Taarifa nyengine iliyopokelewa na Kamati ya Bajeti katika kikao chake na Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi ni Taarifa ya Mashirikiano baina ya SMZ na SMT na Taratibu za Usimamizi wa Uvuvi wa Bahari Kuu. Ambapo Kamati iliarifiwa kwamba, Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi ilifanya kikao cha mashirikiano na Wizara ya Mifugo na Uvuvi ya Serikali ya Muungano wa Tanzania (SMT). Lengo la kikao hicho, ni kuendeleza mashirikiano pamoja na kutatua changamoto zinazozikabili sekta hizo. Kikao kilifanyika Juni 2021.

Katika kikao hicho, mambo ya msingi yaliyowasilishwa, kujadiliwa na hatimae kukubalika ni pamoja na:

i. Leseni zilizotolewa Zanzibar kutambuliwa na kutumika Tanzania Bara

ii. Uvuvi wa "ring net" wakati wa mchana kutoruhusiwa kutumika hususani Tanzania Bara

iii. Wasafirishaji wa dagaa kutoka Zanzibar kwenda nje ya nchi kutozwa ushuru Tanzania Bara (Dar es Salaam na Tunduma)

iv. Usafirishaji wa mazao ya uvuvi ambayo kisheria hayaruhusiwi kuvunwa

Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Serikali ishajihishe taasisi Taasisi za Umma, binafsi na vyuo kufanya tafiti zinazohusiana na sekta zilizopo katika Uchumi wa Buluu.

ii. Licha ya kwamba suala la wasafirishaji wa dagaa kutoka Zanzibar kwenda nje ya nchi limejadiliwa katika kikao cha mashirikiano, Serikali ihakikishe kwamba, changamoto ya wasafirishaji wa dagaa kutoka Zanzibar kutozwa ushuru mara mbili inatafutiwa ufumbuzi kwa haraka.

iii. Kwa upande wa Pemba, bado utekelezaji wa shughuli za Uchumi wa Buluu upo nyuma. Kamati inaishauri Serikali, kutelekeza shughuli hizo pia kwa upande wa Pemba.

## SHIRIKA LA BANDARI LA ZANZIBAR

Shirika la Bandari limeanzishwa rasmi mwezi Julai 1997 chini ya Sheria Nam.1 ya mwaka 1997 na lina jukumu la kuziendesha, kuzisimamia na kuziendeleza Bandari tano za Zanzibar ambazo ni Bandari ya Malindi na Mkokotoni kwa Unguja na Bandari ya Mkoani, Wete na Wesha kwa Pemba.

Kazi za msingi za Shirika ni kutoa huduma za uingiaji na utoaji wa meli Bandarini (Pilotage), ufungaji na ufunguaji wa meli hizo gatini (Mooring/berthing), uangalizi wa alama za kuongozea usafiri wa bahari unaojumuisha minara na maboya (navigation aids), usimamizi wa vyombo vya usafiri wa bahari kwenye maeneo ya Bandari.

Kwa upande wa mizigo na shehena nyenginezo, Shirika lina wajibu wa kuihudumia mizigo hiyo kwa kazi za upakizi (loading), uteremshaji (discharging) na kuihifadhi (Warehousing) katika Bandari zake. Aidha, Shirika linafanya matengenezo ya vyombo vya usafiri wa bahari kwa kutumia Chelezo na Karakana yake kuu ya Malindi (Unguja).

Katika kipindi cha Julai - Septemba 2021 ambacho Kamati ilifanya kazi na Shirika la Bandari, Kamati iliarifiwa kuwa Shirika limetekeleza miradi yake iliyojipangia katika programu tatu ambazo ni: Programu ya Uimarishaji wa miundombinu, Programu ya Ununuzi wa Vitendea kazi na Programu ya TEHAMA ambayo inakusudiwa kupatikana mifumo ya kielektroniki (ePort) kwa ajili ya kuimarisha huduma za Shirika na kuongeza ufanisi.

Changamoto za Shirika

i. Ufinyu wa eneo la kuhifadhia makontena.
ii. Shirika linakabiliwa na tatizo la udogo wa gati ambayo ina urefu wa mita 240 na inaweza kuhudumia meli moja kwa wakati mmoja yenye ukubwa wa mita200.

Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kuwe na mashirikiano baina ya Shirika la Bandari Zanzibar na Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar (ZMA) katika kusimamia mazingira ya bahari. Mathalan, kudhibiti uvujaji wa mafuta kutoka katika meli zinazoingia katika bahari ya Zanzibar.

ii. Mfumo wa TEHAMA unaokusudiwa kutengenezwa na Shirika uunganishwe katika bandari nyengine na sio kuwekwa katika Bandari ya Malindi pekee.

iii. Changamoto za Bandari ya Malindi ambazo ni za muda mrefu zinapelekea kutokuwa na ushindani dhidi ya bandari za jirani. Hali hii inapelekea kukosa mapato mengi hasa ukizingatia kuwa bandari ni sehemu muhimu ya uingizaji mapato ya nchi. Kamati inaishauri Serikali, mbali ya kujenga bandari mpya lakini ihakikishe bandari kwa sasa inafanya kazi kwa ufanisi. Mathalan, kuwepo vifaa vya kutosha vya kushusha na kupakia makontena melini sambamba na kuwepo wafanyakazi wenye weledi.

iv. Ili kupunguza msongomano wa makontena bandarini. Kuwepo na usimamizi mzuri wa makontena katika sehemu ya kuhifadhia na kuhakikisha kuwa makontena yaliyopo ndiyo yanayotakiwa kubakia katika eneo hilo.

## MAMLAKA YA UDHIBITI WA UTAFUTAJI NA UCHIMBAJI WA MAFUTA NA GESI ASILIA ZANZIBAR ( ZPRA)

Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia imeanzishwa chini ya kifungu cha saba (7) cha Sheria ya Mafuta na Gesi Asilia nambari 6 ya mwaka 2016. Mamlaka ina jukumu la kusimamia na kidhibiti shughuli za utafutaji, uendelezaji na uzalishaji wa mafuta na gesi asilia Zanzibar.

### Changamoto za Mamlaka

i. Kamati imebaini katika Mamlaka hakuna uzoefu na utaalamu wa kutosha kuhusu masuala ya mafuta na gesi asilia.

ii. Mamlaka inakabiliwa na uhaba wa fedha na uchelewaji wa upatikanaji wake kutoka Serikalini kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zilizopangwa.

iii. Kukosekana kwa eneo la kudumu la kutunzia taarifa za mafuta na gesi asilia.

Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inaishauri Mamlaka kuusimamia kwa karibu Mpango wa Mafunzo pamoja na miongozo ya kitaalamu inayohusiana na mafuta na Gesi ili uweze kutekelezwa kwa muda uliopangwa.

ii. Kwa kuzingatia kuwa, Mafuta na Gesi ni sekta mpya nchini, Kamati inaitaka Mamlaka kuwapatia uzoefu wafanyakazi wake katika masuala ya Mafuta na Gesi Asilia ili kutekeleza majukumu yao vizuri.

iii. Kamati inaishauri Serikali kuandaa eneo maalum kwa ajili ya kutunza taarifa za mafuta na gesi ili zihifadhiwe vizuri na kuweza kutumika kwa muda wowote pindi zitakapohitajika

iv. Kamati inaitaka Afisi ya Rais Fedha na Mipango kuhakikisha inaipatia Mamlaka fedha kulingana na bajeti yake na kwa muda uliopangwa kwa ajili ya kufanikisha majukumu yake. Aidha, Kamati inaitaka Mamlaka kuwa na vyanzo vya uhakika vya makusanyo ya mapato yanayotokana na shughuli za mafuta na Gesi Asilia

v. Kamati inaitaka Serikali kusaidia suala la upatikanaji wa taarifa za mafuta na gesi zilizohifadhiwa katika Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) ili ziweze kusaidia katika utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka.

## KITENGO CHA MADENI CHA AFISI YA RAIS FEDHA NA MIPANGO

Kamati ya Bajeti ilipata fursa ya kukutana na Kitengo cha Madeni na kujadiliana mambo mbali mbali ikiwemo majukumu ya kitengo, changamoto na mafanikio yaliyopatikana.

Miongoni mwa majukumu yake ni pamoja na kuweka kumbukumbu za madeni ya ndani na ya nje pamoja na dhamana zinazotolewa na Serikali kwa taasisi za Serikali, kuainisha na kuorodhesha madeni ya mikopo na riba zilizoiva kwa ajili ya

kuwezesha ulipaji kwa wakati.

### Changamoto za Kitengo

i. Kuchelewa kufanya usuluhishi wa madeni (Debt Reconciliation) kati ya taarifa za Serikali ya Jamhuri ya Muungano Tanzania (SMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ).

ii. Uelewa mdogo wa taasisi katika kufuata utaratibu wa kukopa au kuomba dhamana ya Serikali inayopelekea maombi kuchukua muda mrefu hadi kukamilika kwake.

### Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inaitaka Afisi ya Rais Fedha na Mipango kuendelea kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kufanya usuluhishi wa Deni la Taifa kwa wakati kwa kulinganisha taarifa zilizopo kwa pande zote mbili za Muungano.

ii. Kamati inaishauri Afisi ya Rais kutoa mafunzo kwa taasisi za Serikali ili kupata uelewa mpana wa taratibu za kukopa na kuomba dhamana katika madeni.

iii. Kamati inashauri katika mfumo uliopo wa kuweka kumbukumbu za madeni ya Taifa, kusimamiwa vizuri taarifa zake ili ziweze kutumika muda wote zitakapohitajika.

## BODI YA MAPATO ZANZIBAR (ZRB)

Katika utekelezaji wa majukumu yake ya kufuatilia ukusanyaji wa mapato Kamati ya Bajeti ilifuatilia utekelezaji wa shughuli za Bodi ya Mapato Zanzibar ili kutathmini namna Bodi hiyo inavyotekeleza majukumu yake ya ukusanyaji wa kodi. Mapato yanayopatikana yanasaidia sana katika utekelezaji wa shughuli za

Serikali ikiwemo utoaji wa huduma bora kwa wananchi.

Changamoto za Bodi

i. Kamati imebaini kuwepo kwa upungufu wa wataalamu wa kuandaa mfumo wa utowaji wa risiti za mtandao (Virtual Fiscal Management System –VFMS) ambao hutumika kwa ajili ya kukusanya mapato yanayotokana na Kodi. Mfumo huo umeandaliwa na wataalamu watano ambapo wawili ni watendaji wa Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) na watendaji wengine watatu wameazimwa kutoka taasisi nyengine za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
ii. Kamati imebaini kuwa, Mfumo wa utowaji wa risiti za mtandao (Virtual Fiscal Management System –VFMS) unahitaji kuimarishwa zaidi kwa kuhakikisha kuwa taarifa zote zinazohitajika zinaingizwa kwa wakati pamoja na kuunganisha mfumo huu na mifumo mengine ya taasisi za Serikali hasa katika kupata taarifa za mteja (ZAN ID).
iii. Upungufu wa fedha katika kutekeleza majukumu yao hasa majukumu ya kiutendaji yanayohusisha kazi za kitaalamu zikiwemo za kuandaa mifumo ambazo mafanikio yake zinategemea pia uwepo wa rasilimali fedha na rasilimali watu.
iv. Kamati imebaini kuwa, mtendaji mmoja aliyepo katika kituo cha Huduma na Mawasiliano kwa Walipa kodi (ZRB Contact Centre) hatoshelezi kwani majukumu yaliyopo katika kituo hicho yanahitaji watendaji zaidi ya mmoja katika kufanikisha kazi za kituo kwa ufanisi.
v. Kamati imebaini kuwa Mapato ya Mawizara kwa kipindi cha Julai –Septemba 2021/2021 ambayo makusanyo yake yalikuwa yanasimamiwa na Bodi ya Mapato ya Zanzibar (ZRB), kwa sasa mapato hayo hayakuainishwa katika taarifa ya ZRB na Kamati haikupatiwa ufafanuzi wa taasisi inayohusika kutoa taarifa ya makusanyo hayo.
vi. Kamati imebaini kuwa mfumo wa utowaji wa risiti za mtandao (Virtual Fiscal Management System –VFMS) haujafikia makundi yote ya walipa kodi ambapo kwa sasa waliofikiwa wengi ni wafanyabiashara ambao ni wamiliki

wa mahoteli makubwa yaliyopo Zanzibar.

Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inaishauri Serikali kusaidia katika upatikanaji wa fedha za kutosha kwa ajili ya kusimamia uanzishwaji wa mifumo ya mtandao nchini kwa kuwatumia wataalamu wa ndani ambao ni wazalendo na pia wenye uwelewa mpana wa mazingira ambayo mifumo mbali mbali itahitaji kutayarishwa.

ii. Kamati inaipongeza Bodi ya Mapato ya Zanzibar kwa kufanikiwa kuandaa Mfumo wa utowaji wa risiti za mtandao (Virtual Fiscal Management System –VFMS) ambao utasaidia katika kufanikisha majukumu yao. Aidha Kamati inaitaka Bodi kuendelea kutoa elimu kwa jamii juu ya umuhimu wa kutoa na kudai risiti wakati wa kununua na kuuza bidhaa mbali mbali.

iii. Kamati inashauri wataalamu walioandaa mfumo wa VFMS kujitahidi katika kuhakikisha kuwa taarifa zote zinazohitajika kuingizwa katika mfumo huo zinaingizwa moja kwa moja (automatic) badala ya kuingiza kwa utaratibu mwengine (manual) hali inayoweza kupelekea kupungua ubora wa mfumo huu.

iv. Licha ya kuwa kituo cha Huduma na Mawasiliano kwa Walipa kodi (ZRB Contact Centre) kipo katika hatua za majaribio, Mtendaji mmoja aliyekuwepo hatoshelezi na hivyo, Kamati inashauri Bodi kuandaa watendaji wa kutosha wa kuhudumia kituo hicho ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

v. Katika kuhakikisha mapato ya kodi yanaongezeka, Kamati inaishauri Bodi kupanua wigo wa watumiaji wa Mfumo wa utowaji wa risiti za mtandao (Virtual Fiscal Management System –VFMS) katika ukusanyaji wa mapato.

vi. Kamati inaiagiza Afisi ya Rais, Fedha na Mipango kuitambua taasisi inayosimamia mapato ya Mawizara ili taasisi hiyo iweze kuhojiwa mapato hayo katika utekelezaji wa shughuli zilizopangwa.

vii. Kamati inaishauri Serikali, kuhakikisha taarifa zote za mapato yasiyokuwa ya kodi ya mawizara zinapelekwa Bodi ya Mapato Zanzibar kwa ajili ya

kurahisisha utoaji wa taarifa za mapato.

## MAMLAKA YA VIWANJA VYA NDEGE ZANZIBAR (ZAA)

Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar imeanzishwa kwa Sheria namba 8 ya mwaka 2011. Miongoni mwa majukumu yake ni pamoja na kuviendesha, kuvisimamia na kuviendeleza viwanja vya ndege vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kusimamia usalama wa safari za abiria na mizigo katika viwanja vya ndege vya Serikali. Kamati ilipokea taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka na kuona mafanikio, changamoto na kutoa maoni kwa ajili ya utekelezaji bora wa shughuli za Mamlaka.

### Changamoto za Mamlaka

i. Kamati haikuridhishwa na kiwango cha fedha cha shilingi elfu mbili kwa saa kwa gari za kawaida ambapo kiwango hicho ni kikubwa. Aidha, Kamati haijaridhishwa na utaratibu unaotumika katika kukusanya tozo za vyombo vya moto vinavyoingia katika Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar ambapo risiti za malipo huandaliwa kabisa kabla ya mteja kufika na kupatiwa hali inayotia shaka katika ukusanyaji wa mapato hayo.

ii. Ufinyu wa maeneo katika jengo la Terminal 3 kunapelekea kuwepo kwa changamoto katika matumizi ya kiwanja hicho kipya ikiwemo msongamano wa abiria wa kimataifa na kupelekea abiria hao kuwekwa katika mahema kwa ajili ya kusubiria huduma.

iii. Licha ya watendaji kupatiwa mafunzo kwa kada mbali mbali, bado hayajafikia katika kiwango kinachohitajika. Watendaji wa mamlaka ya viwanja vya ndege pamoja na wadau wake wanatakiwa kuelimishwa juu ya matumizi sahihi ya vifaa na mitambo mbali mbali iliyopo katika kiwanja hicho.

### Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inaishauri Mamlaka iandae mfumo maalumu ambao ndio

utakaotumika katika kukusanya mapato ya vyombo vya moto vinavyoingia katika maegesho ya viwanja vya ndege. Utaratibu uliopo wa kuandaliwa risiti kabla ya mteja kufika katika eneo husika la kupatiwa huduma unatia wasi wasi mkubwa Kamati na kuhofia kuvuja kwa baadhi ya mapato.

ii. Kamati inaitaka Mamlaka kusimamia vyema ukodishwaji wa maduka na kuhakikisha kuwa, taratibu zote zinafuatwa ikiwemo za kimkataba.
iii. Kamati inaitaka Mamlaka kuendelea na usimamizi madhubuti wa mafunzo kwa watendaji kwa kuzingatia mahitaji mbali mbali ya jengo hilo jipya ili mafunzo hayo yasaidie katika utekelezaji wa majukumu yao kwa ufanisi.

## SHIRIKA LA BIASHARA LA TAIFA ZANZIBAR (ZSTC)

Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC) ni miongoni mwa mashirika yanayomilikiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na miongoni mwa majukumu yake ni pamoja na kununua na kuuza karafuu na mazao mengine ya kilimo na kufanya usarifu na kuongeza thamani ya karafuu na mazao mengine ya kilimo.

### Changamoto za Shirika

i. Kamati imebaini kuwa, Shirika linakabiliwa na uhaba wa fedha kwa ajili ya ununuzi wa karafuu hali inayopelekea Shirika kuingia katika mikopo yenye riba kubwa kwa ajili ya ununuzi wa zao hilo
ii. Kushuka bei ya karafuu katika soko la dunia inaathiri mapato ya Shirika. kwa mwaka wa 2020/2021 Shirika lilinunuwa karafuu kutoka kwa mkulima kwa wastani wa TZS 14,000 kwa kilo wakati mauzo ya karafuu duniani ni wastani wa USD 4 kwa kilo ambazo ni sawa na TZS 9,400 ambapo katika hali hii Shirika linafanya biashara kwa hasara.
iii. Shirika linakabiliwa na madeni makubwa ya fedha kutoka taasisi mbali

mbali ikiwemo PBZ na ZSSF. Aidha, Shirika linadaiwa karafuu kwa baadhi ya wateja wake ambao waliingiza fedha katika mwaka wa 2020/2021 kwa ajili ya kupatiwa karafuu.

iv. Kutokana na uhaba wa fedha za Shirika, imepelekea kushindwa kulipa madeni katika utekelezaji wa miradi yake. Katika ujenzi wa kitega uchumi Malindi, kampuni ya ZECON Construction inaidai Shirika kiasi cha TZS 208.75 milioni.

v. Kamati imebaini kusuasua kwa baadhi ya Miradi ya Shirika la ZSTC kutokana na ukosefu wa fedha, ikiwemo Mradi wa maghala ya kununulia na kuhifadhia karafuu ambao Mkandarasi ameshindwa kuendeleza kwa kutumia fedha zake.

Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati imebaini kuuza karafuu zikiwa malighafi haingizii mapato ya kutosha Shirika, Hivyo, inaitaka Serikali kuangalia mbinu nyengine mbadala ambayo itapelekea kuingiza kipato cha kutosha Shirika ikiwemo usarifu wa zao hilo ili kuuza bidhaa nje ya nchi badala ya malighafi.

ii. Kwa kuwa uendeshaji wa Shirika si wa ufanisi, Kamati inaitaka Wizara kulifanyia kazi tatizo hili na kuchukuliwa hatua za haraka za kulinusuru Shirika.

iii. Changamoto ya uhaba wa fedha katika Shirika unakwaza utekelezaji wa majukumu yao, hivyo Kamati inaishauri Serikali kuliangalia Shirika hili kwa karibu na kuweza kulisaidia.

iv. Kutokana na kusuasua kwa biashara ya zao la Karafuu kunakosababishwa na kushuka kwa bei ya zao hilo katika soko la dunia, Kamati inalishauri Shirika kutafuta fursa zaidi za biashara katika bidhaa nyengine za kilimo ikiwemo zao la mwani ambalo wananchi kwa muda mrefu wamekuwa wakihitaji soko la uhakika la bidhaa hiyo.

v. Kamati imebaini Mfuko wa Maendeleo ya Karafuu ambao umeanzishwa kisheria, hauchangiwi na wadau waliotajwa katika sheria, Kamati inaishauri Serikali kukaa na Shirika kuitafutia ufumbuzi changamoto hiyo.

vi. Kamati imebaini Kiwanda cha Makonyo kinakabiliwa na changamoto ya uchakavu wa mitambo na pia kinatumia teknolojia ya kizamani ambayo inapunguza ufanisi na pia inaweza kupelekea uchafuzi wa mazingira. Kamati inaishauri Serikali kukiwezesha Kiwanda kuwa na ubunifu kwa kutumia njia za kisasa za uzalishaji husasani katika matumizi ya nishaji bora.

## WIZARA YA AFYA, USTAWI WA JAMII, WAZEE, JINSIA NA WATOTO

Kamati ya Bajeti katika Wizara hii kwa upande wa Pemba, ilitembelea Mradi wa Upanuzi wa Hospital ya Wete ambao makubaliano yake yalianza mwaka 2018 baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Falme za Kiarabu na kutiwa saini mwezi September, 2019. Mradi huu unahusisha majengo mapya na kufanya ukarabati wa majengo ya zamani. Mradi utagharimu jumla ya dola ya kimarekani milioni kumi (USD 10 milioni) ikiwa ni msaada kutoka Serikali ya Abu Dhabi. Katika mwaka wa fedha wa 2021/22, mradi umepangiwa jumla ya TZS 7 bilioni ambapo kati ya fedha hizo, TZS 6.9 bilioni sawa na asilimia 98.6 kutoka Serikali ya Abudhabi na TZS 100 milioni sawa na asilimia 1.4 kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Kamati imeelezwa kuwa mradi huu upo katika hatua za awali. Kazi zilizofanyika ni pamoja na kutambuliwa eneo la mradi, kupimwa na kufanyika kwa uchuguzi wa udongo. Eneo lina ukubwa wa mita za mraba 35,219 na lipo katika hatua ya kupatiwa usajili. Mradi utakapokamilika utapelekea kuongeza idadi ya vitanda vya Hospitali kutoka 140 hadi kufikia vitanda 240.

Kwa upande wa ujenzi wa Uzio wa Hospitali ya Chake Chake ulioanza mwaka 2011 kupitia Programu ya Uratibu wa shughuli za Afya Pemba ambapo fedha zake zilitengwa katika bajeti ya 2019/2020 na bajeti ya 2020/2021. Kamati ilipotembelea mradi ilibaini kuwa, hospitali hiyo haijazungushiwa uzio kwa maeneo yote, isipokuwa uzio umezungushwa katika baadhi ya sehemu za hospitali na hivyo mradi haukutelezwa kwa kiwango kilichokusudiwa.

Pia, katika Wizara hii, Kamati ilipata fursa ya kutembelea Kituo cha Uchukuaji wa

Sampuli za Korona Mfikiwa  - Pemba.

Changamoto zilizopo katika Kituo cha Uchukuaji za Sampuli za KORONA- Pemba

i. Kituo cha Uchukuaji wa Sampuli za Korona cha Mfikiwa – Pemba hakina ofisi za kudumu kwa ajili ya kufanya huduma zake hali inayowalazimu kuendelea kutumia jengo la kuazima la Shirika la Red Cross kwa ajili ya kuchukua sampuli za washukiwa kutoka hospitali zote za Pemba na vituo vya afya vitatu (teule) kwa kila Wilaya na.
ii. Kutokuwa na fungu maalum la fedha kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za Kitengo hali inayopelekea shughuli muhimu za kitengo hicho ikiwemo uchukuaji wa sampuli kutoka Pemba na kuziwasilishwa Unguja katika maabara ya Hospitali ya Mnazi Mmoja na kufanyika kwa makubaliano na mashirika ya ndege kusaidia kuchukua sampuli hizo bila ya gharama yoyote.
iii. Kitengo kukosa usafiri kwa ajili ya shughuli zake mbali mbali za ufuatiliaji.

Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inaishauri Serikali katika bajeti ya mwaka wa fedha 2022/23 kuitengea fedha maalum Wizara kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha uchukuaji wa sampuli za KORONA - Pemba, ili watendaji wapate maeneo mazuri  na ya uhakika kwa ajili ya kufanya majukumu yao.
ii. Kamati inaitaka Wizara kusimamia upatikanaji wa fungu maalum la fedha kwa ajili ya Kituo cha uchukuaji wa sampuli za korona ili kituo kitekeleleze majukumu yake vizuri.
iii. Licha ya kuwa, Mradi wa Upanuzi wa Hospitali ya Wete kuwa katika hatua za awali, Kamati inasisitiza juu ya upatikanaji wa fedha kama ilivyokusudiwa kwa upande wa Serikali na Washirika wa Maendeleo ili mradi uweze kutekelezwa na kukamilishwa katika muda uliyokusudiwa.

## WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA UCHUKUZI

Kamati ilipokea taarifa ya utekelezaji wa miradi mbali ya uimarishaji wa miundombinu ya barabara na huduma za usafirishaji iliyohusisha miradi ya uimarishaji wa miundombinu ya barabara, Miradi ya Uimarishaji wa Usafiri wa Anga na Miradi ya Uimarishaji wa Usafiri Baharini. Aidha, Kamati ilipokea taarifa za utekelezaji kazi za Wakala wa barabara kwa kipindi cha Julai – Disemba 2021.

### Changamoto za Wizara

i. Kamati imebaini kuwa kwa kipindi cha Julai – Disemba 2021, baadhi ya miradi ya uimarishaji wa miundombinu ya barabara imeshindwa kutekelezwa kabisa kutokana na kukosekana kwa fedha, miongoni mwa miradi hiyo ni pamoja na Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Jozani – Charawe – Ukongoroni (Km 23), Ujenzi wa Barabara ya Kizimbani – Kiboje (Km 7.2) na Ujenzi wa Barabara ya Jumbi Sokoni - Tunguu (Km 4).

ii. Katika utekelezaji wa Mradi wa Uimarishaji wa Usafiri wa Anga, hakuna kazi iliyotekelezwa kwa uwanja wa ndege Pemba kwa kipindi cha Julai – Disemba 2021 kutokana na kukosekana kwa fedha za utekelezaji.

iii. Wakala wa Barabara kushindwa kutekeleza shughuli zilizokusudiwa ikiwemo ujenzi wa msingi wa maji ya mvua katika eneo la Mfenesini Unguja (0.4 Km ) na ujenzi wa daraja la Machui – Unguja kutokana na kukosekana kwa fedha za utekelezaji wa shughuli hiyo.

iv. Wakala kushindwa kutekeleza ujenzi wa daraja la Vitongoji - Pemba kutokana na kutokukamilika kwa taratibu za kazi husika.

### Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inaishauri Serikali kuingiza fedha za bajeti kwa wakati ili utekelezaji wa kazi mbali mbali zilizopangwa uweze kufikiwa.

ii. Kamati inashauri watendaji kufuatilia taratibu za utekelezaji wa miradi ili miradi hiyo iweze kutekelezwa zinapopatikana fedha za utekelezaji.

## MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA - TAWI LA ZANZIBAR

Kamati ya Bajeti katika kutekeleza majukumu yake ilitembelea Mamlaka ya Mapato Tanzania, Tawi la Zanzibar na kupokea Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Mamlaka hiyo ikiwemo taarifa ya ukusanyaji wa mapato kwa kipindi cha miezi sita, Julai - Disemba, 2021. Katika kipindi hicho, Mamlaka ilipangiwa kukusanya jumla ya TZS 201.4 bilioni, mapato halisi yaliyokusanywa na Mamlaka ni TZS 165.16 bilioni sawa na utekelezaji wa asilimia 82 ya makisio ya kipindi hicho.

### Changamoto za Mamlaka

i. Kupungua kwa mapato yanayotokana na sekta ya utalii katika kipindi hichi cha miezi sita, ukusanyaji mapato wa sekta hii bado haijaimarika sana kutokana na janga la UVIKO 19.
ii. Ushirikiano mdogo kwa taasisi za Serikali katika kutoa taarifa mbali mbali kwa wakati ikiwemo za walipa kodi kunatoa fursa kwa baadhi ya wafanyabiashara kukwepa ulipaji wa kodi.
iii. Ujuzi mdogo kwa watumishi wa Mamlaka katika fani ya utozaji kodi kwa kampuni za kimtaifa zinazofanya biashara zake nchini Zanzibar (International Taxation).
iv. Kukosekana kwa muda wa kutosha wa kuwajengea uwezo wafanyakazi wapya katika kupata uzoefu kutoka kwa watumishi wa zamani. Hali hii inachangiwa na kasi ya kustaafu wataalamu wenye ujuzi ni mkubwa ukilinganisha na mwenendo wa ajira mpya.
v. Ufinyu wa nafasi katika Bandari ya Zanzibar na msongamano wa meli za mizigo zinazoingia nchini kunapelekea kupungua kwa kasi ya uteremshaji wa makontena na hivyo kuathiri biashara na malipo ya kodi.
vi. Wananchi bado wana uelewa mdogo katika ulipaji wa kodi kwa hiari.
vii. Ukusanyaji wa kodi kwa wafanyakazi wataalamu wa kigeni wanaoajiriwa kupitia sekta mbali mbali hauendi sambamba na uhalisia wa mishahara wanaolipwa.

viii. Kuwepo kwa tofauti za sera na vipaumbele baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kunachangia ugumu katika kuweka uwiano baina ya matakwa ya kila Serikali katika usimamizi wa kodi

Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inaishauri Mamlaka kuendelea na utaratibu wa kuielimisha jamii juu ya umuhimu wa kulipa kodi kwa hiari na namna mapato yake yanavyosaidia katika uchumi wa nchi.
ii. Kamati inaishauri Mamlaka kwa kushirikiana na Uongozi wa Shirika la Bandari Zanzibar kuipatia ufumbuzi changamoto ya uhaba wa vifaa vya kushushia kontena ili kuondokana na mrundikano wa makontena katika bandari na kupelekea mizigo kushushwa kwa wakati sambamba na ukusanyaji wa kodi katika muda unaostahiki.
iii. Kamati inashauri kuwepo kwa mashirikiano ya karibu kwa taasisi mbali mbali ikiwemo benki, taasisi zinazosajili biashara na Wizara katika kutoa taarifa zinazohusiana na ukusanyaji wa kodi.
iv. Kamati inaishauri Mamlaka kuwapatia watendaji mafunzo mbali mbali kwa ajili ya kujenga uzoefu na uweledi katika kutekeleza majukumu yao.

## WAKALA WA MAENDELEO YA VIWANDA VIDOGO VIDOGO NA VYA KATI (SMIDA)

Kamati katika kutekeleza majukumu yake ilipata fursa ya kukutana na Wakala wa Maendeleo ya Viwanda vidogo vidogo na vya Kati (SMIDA) kwa lengo la kupokea taarifa ya utekelezaji wa majukumu yao ikijumuisha mapato na matumizi kuanzia mwaka 2018/2019 mpaka 2020/2021, changamoto na mafanikio yaliyopo katika utekelezaji wa majukumu yao.

Katika utekelezaji wa majukumu yao kwa kipindi cha miaka mitatu 2018/2019 – 2020/2021 Wakala ilitengewa jumla ya TZS 6,250,052,301, kati ya fedha hizo TZS 3,124,052,301 kwa ajili ya shughuli za miradi ya maendeleo (ujenzi wa makao

makuu ya SMIDA) na TZS 3,126,000,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Fedha halisi zilizopatika na kwa kipindi hicho kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za kawaida za Wakala ni TZS 1,801,916,307 na matumizi yaliyofanyika katika fedha hizo ni TZS 336,000,000 ukarabati mkubwa wa majengo yanayotumika kwa ajili ya Ofisi za SMIDA Unguja na Pemba, ununuzi wa vyombo vya usafiri  na TZS 1,195,916,307 zimetumika kutekeleza majukumu na kazi mbali mbali za SMIDA.

Changamoto zilizopo SMIDA

i. Upungufu wa wafanyakazi wenye sifa hasa wahandisi kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za Divisheni ya karakana na Divisheni ya Teknolojia. Kamati ilipotembelea Ofisi za Wakala ilielezwa kuwa,wahandisi waliopo ni watatu (3) wakati mahitaji halisi ya wahandisi katika fani mbali mbali za uhandisi ni  kumi na sita (16)
ii. Wakala wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo vidogo na vya Kati inakabiliwa na upatikanaji mdogo wa fedha ambapo kwa kipindi cha miaka mitatu ilipatiwa asilimia 38.9 tu ya fedha zote ilizozihitaji kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zake.
iii. Kamati ilielezwa kuwa, Wakala wanakabiliwa na ukosefu wa maeneo maalum ya uzalishaji (common facilities) yenye miundombinu na dhana sahihi za uzalishaji. Kamati ilipokuwa inapokea taarifa ilielezwa kuwa, Wakala hawana hata eneo moja lenye sifa, miundombinu, vifaa, zana na nyezo za uzalishaji hali inayopelekea wajasiriamali wadogo kushindwa kuendelea na uzalishaji, kutokana na kukosa maeneo.
iv. Kukosekana kwa Karakana kwa ajili ya kutoa huduma za matengenezo ya mashine na vipuri hali inayopelekea kuongezeka kwa idadi ya mashine ambazo zimeshindwa kutumika kwa ajili ya uzalishaji. Aidha, Kamati imeelezwa juu ya kukosekana kwa ubunifu katika uzalishaji hali inayochangia bidhaa kukosa soko.
v. Kukosekana kwa mifumo ya TEHAMA itakayosaidia katika uendeshaji wa shughuli za Wakala ikiwemo utowaji na usimamizi wa mikopo jambo

linalopelekea mikopo inayotolewa kutosimamiwa vizuri.

vi. Ukosefu wa vitendea kazi ikiwemo usafiri kunazorotesha shughuli za utendaji ikiwemo kufuatilia mikopo, usambazaji wa barua na ufuatiliaji wa maendeleo ya miradi ya viwanda. Kamati iliarifiwa kuwa, gari iliyopo ni moja tu ambayo hutumika kwa kazi zote za ofisi.

Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inaishauri Serikali kupitia vyombo vyake na taasisi mbali mbali kushirikiana kwa pamoja katika kuweka mikakati ya kuondosha changamoto mbali mbali inazozikabili Wakala ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na azma ya Serikali ya kuona mchango wa viwanda katika maendeleo ya nchi inafikiwa.

ii. Kamati inasisitiza Wakala juu ya umuhimu wa kuwapatia mafunzo wajasiriamali ili mafunzo hayo yaweze kuwasaidia katika shughuli zao pamoja na kuwaendeleza wabunifu wa ndani ili waweze kubakia na kuendelea na shughuli zao za uzalishaji nchini.

iii. Kamati inashauri Wakala, katika jitihada ya kukabiliana na mikopo isiyorejeshwa kwa wakati na wajasiriamali, kuandaa kanuni madhubuti zitakazoeleza wazi masharti na muda wa kurudisha mikopo hiyo ili wajasiriamali wengine waweze kufaidika na mikopo hiyo.

iv. Kamati inaitaka Wakala kuendelea na shughuli ya kuwatafutia masoko wajasiriamali ili bidhaa zinazozalishwa na wajasiriamali ziweze kuuzwa katika masoko ya ndani na nje.

v. Kamati inaitaka wakala kubuni miradi ya kuongeza thamani bidhaa mbali mbali zinazozalishwa nchini ikiwemo karafuu, mwani na madagaa ili kuondokana na tatizo na kuuza bidhaa hizi kwa bei isiyoridhisha.

# SEHEMU YA TANO

## UCHAMBUZI WA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU NA BAJETI YA MAMLAKA YA SERIKALI ZA MITAA

Kamati ya Bajeti katika kutambua na kuthamini mchango wa Serikali za Mitaa katika utekelezaji wa shughuli zake na uchangiaji wake katika shughuli za maendeleo ilipokea taarifa za mapato na matumizi ya Baraza la Mji Chake Chake, Baraza la Mji Mkoani, Baraza la Mji Wete na Halmashauri ya Micheweni kwa upande wa Pemba na Baraza la Mji Kaskazini “A” na Baraza la Mji Kaskazini “B” kwa upande wa Unguja, kwa mwaka wa fedha 2020/2021 na kwa kipindi cha Julai - Disemba 2021/2022. Taarifa hizo za mapato na matumizi ya Mabaraza ya Miji na Halmashauri pia zilijumuisha taarifa zifuatazo:

i. Taarifa ya uchambuzi wa mapato kutoka katika vyanzo vyote Baraza la Mji/Halmashauri.

ii. Taarifa ya uchambuzi wa matumizi kwa shughuli zote za Baraza la Mji/Halmashauri zilizofanywa.

iii. Mafanikio na changamoto katika ukusanyaji wa mapato, uibuaji wa vyanzo vipya vya mapato na utekelezaji wa bajeti kwa Baraza la Mji/Halmashauri.

iv. Taarifa za zabuni zilizotolewa na Baraza la Mji/Halmashauri zikiwemo zabuni za kufanya usafi wa miji, maegesho ya gari na zabuni nyenginezo.

v. Taarifa ya kuunganishwa mifumo ya mapato ya Baraza la Mji/Halmashauri katika mfumo wa ZanMalipo.

vi. Mpango kazi wa Baraza la Mji/Halmashauri kwa mwaka wa fedha

2021/2022

**Changamoto ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mabaraza ya Miji na Halmashauri ya Unguja na Pemba**

i. Kutopatiwa ruzuku ya matumizi mengineyo kwa baadhi ya Mabaraza na Halmashauri.

ii. Matumizi kwa miradi ya maendeleo hayaridhishi, matumizi mengi yanakwenda kwenye shughuli za uendeshaji wa ofisi.

iii. Vyanzo vya mapato vya mabaraza kusimamiwa na taasisi nyengine kama vile mapato ya vibali vya ujenzi, maliasili na vituo vya mafuta.

iv. Kuchelewa kwa marejesho ya mapato kutoka Kamati ya Usimamizi na Udhibiti wa Ujenzi Zanzibar (DCU), Idara ya Maliasili, ZURA na Bodi ya Vileo.

v. Upungufu wa watumishi wenye weledi katika maeneo ya ukusanyaji wa mapato

vi. Mfumo wa kukusanyia mapato wa ZanMalipo kuwa na changamoto mbalimbali zikiwemo za ukosefu wa POS za kutosha na hitilafu za kimtandao.

vii. Kukosekana kwa vyanzo vya kudumu vya mapato vinavyotokana na miradi ya kiuchumi iliyoanzishwa na Mabaraza au Halmashauri.

**Maoni na Ushauri wa Kamati Mabaraza ya Miji na Halmashauri ya Unguja na Pemba**

i. Kamati inayasisitiza Mabaraza ya Miji na Halmashauri kuendelea kusimamia vizuri ukusanyaji wa mapato ili kufikia lengo lililokusudiwa.

ii. Kamati inayashauri Mabaraza ya Miji na Halmashauri kusimamia matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato ili kudhibiti upotevu wa mapato hayo.

iii. Kamati inayashauri Mabaraza ya Miji na Halmashauri kuhakikisha wanatenga fedha za kutosha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo kwa jamii ili mapato yanayokusanywa kwa wananchi yaweze kuwaondolea kero mbalimbali za kijamii na kiuchumi zinazowakwaza katika maisha ya kila siku.

iv. Kamati inaishauri Serikali kuajiri vijana wenye sifa kwa lengo la kuzisaidia Mamlaka hizi katika uendeshaji wa shughuli zake ili zifikie malengo waliojiwekea.

v. Kamati inaishauri Serikali kuwayapatia ruzuku stahiki Mabaraza ya Miji.

vi. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuishajihisha jamii katika kudai risiti pindi wanapotozwa tozo na ada mbali mbali.

vii. Kamati inaishauri Serikali kusimamia marejesho ya mapato ya Mabaraza yaliyokusanywa na DCU, ZURA na Idara ya Maliasili.

### Maoni na Ushauri wa Jumla wa Kamati kwa Mabaraza ya Miji, Halmashauri na Manispaa za Zanzibar

Kamati imebaini kwamba Mabaraza na Halmashauri zinatofautiana vyanzo vya ukusanyaji mapato licha ya kwamba upo uwezekano wa kutekelezeka vyanzo vinavyolingana katika Mabaraza na Halmashauri zote. Hali hii inatokana na kukosekana kwa mazingatio mazuri kwa baadhi ya vyanzo vya mapato au kutoripotiwa kwa taarifa za mapato kutoka katika vyanzo hivyo. Kamati inaishauri Serikali, kukaa na Mabaraza ya Miji, Halmashauri na Manispaa zote za Zanzibar na kuorodhesha vyanzo vyote vya mapato vinavyoweza kukusanywa na Baraza, Halmashauri au Manispaa husika pamoja na kuweka makisio ya makusanyo kwa kila chanzo. Taarifa ya vyanzo vyote vya mapato na makadirio yake kwa kila Baraza, Halmashauri na Manispaa yawekwe katika Hotuba ya Bajeti kila mwaka.

# SEHEMU YA SITA

## UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO NA PROGRAMU MBALI MBALI

### Ushiriki wa Sekta Binafsi katika kufadhili Miradi ya Maendeleo.

Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ni njia mbadala ya kufadhili miradi ya maendeleo ambayo inazalisha faida ili Serikali ijikite kwenye maeneo mengine ambayo hayavutii Sekta Binafsi kuwekeza. Ushiriki wa Sekta binafsi katika miradi ya maendeleo unapunguza gharama ya Serikali katika kugharamia miradi hiyo na pia inachochea kwa kiasi kikubwa katika ukuaji wa uchumi.

### Changamoto

Ili kuwezesha kuimarika kwa sekta binafsi, Serikali ihakikishe inasaidia kutatua changamoto zinazoikabili sekta hiyo. Miongoni mwa changamoto zinazoikabili

sekta binafsi ni:-

i. Wingi wa mamlaka za udhibiti zinazosimamia shughuli za sekta binafsi.
ii. Ugumu katika upatikanaji wa mikopo na uwepo wa riba za juu na ucheleweshaji wa utolewaji wa maamuzi.
iii. Wingi wa leseni, tozo na ada kwenye biashara moja.
iv. Kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara na uwekezaji.

Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Ili kurahisisha ukusanyaji wa mapato na kuwaondeshea usumbufu wafanyabiashara wa kuwepo utitiri wa mamlaka za udhibiti na wingi wa tozo na kodi, Kamati inashauri kuwepo mamlaka moja au chache za udhibiti wa biashara na kuwepo kodi moja ambayo baadae kila mamlaka husika ipate mgao wake.
ii. Kamati inashauri kuimarishwa maeneo ya ufanyaji biashara na uwekezaji.

## MIRADI YA MAENDELEO ILIYOFANYIWA KAZI NA KAMATI YA BAJETI

Kamati ya Bajeti ilipokea taarifa za miradi ya maendeleo mbali mbali ambazo ilizichambua kwa kina na kuikagua miradi hiyo na hatimae kutoa maoni na ushauri kwa taasisi zinazotekeleza miradi hiyo. Miradi hiyo ya maendeleo iliyofanyiwa kazi na Kamati ni kama ifuatavyo:

### MRADI WA ELIMU YA LAZIMA KUPITIA MRADI MDOGO WA KUIMARISHA ELIMU YA SEKONDARI (ZANZIBAR IMPROVING STUDENT PROSPECTS - ZISP)

Mradi wa Elimu ya Lazima Kupitia Mradi Mdogo wa Kuimarisha Elimu ya Sekondari (ZISP) ulikuwa ni mradi wa miaka mitano kuanzia 2016/2017 hadi 2020/2021. Kwa sasa mradi umeongezewa muda wa miezi 18 na hivyo utakamilika rasmi mwezi 2023. Mradi huu utagharimu jumla ya Dola za Kimarekani 35 milioni mpaka kukamilika kwake, fedha hizi ni mkopo kutoka Benki ya Dunia (WB).

Hadi Juni 2021, jumla ya Dola za Kimarekani 25.6 milioni sawa na asilimia 73.1 zimetumika tokea kuanza kwa mradi.

### Changamoto za Mradi

i. Mripuko wa ugonjwa wa UVIKO 19 uliathiri kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa mradi kwani ilipelekea kusitishwa kwa mafunzo pamoja na kuondoka na kuchelewa kurudi mshauri mwelekezi.

### Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Panapokuwa na changamoto zozote kama vile mripuko wa UVIKO 19, kuwepo na njia mbadala za kuhakikisha miradi inatekelezwa kama ilivyopangwa.

## MRADI WA UKUZAJI UCHUMI JUMUISHI ZANZIBAR (BOOSTING INCLUSIVE GROWTH FOR ZANZIBAR-BIG Z)

Mradi wa Ukuzaji Uchumi Jumuishi Zanzibar (Boosting Inclusive Growth for Zanzibar, BIG-Z) uliidhinishwa rasmi Juni 2021 na kusainiwa Agosti 2021 na unafadhiliwa na Benki ya Dunia (WB). Mradi huu utagharimu Dola za Kimarekani milioni 150 na unatarajiwa kutekelezwa kwa muda wa miaka mitano, yaani 2021/2022 hadi Juni 2026/2027. Mradi unakusudiwa kuimarisha miundombinu na utoaji wa huduma kwa jamii, uhifadhi wa urithi na usimamizi jumuishi wa Miji ya Zanzibar.

### Changamoto za Mradi

i. Kuchelewa kwa fedha kutoka Benki ya Dunia kutokana na hatua za kibenki zinazohitajika kufanywa kabla ya fedha hizo kutoka.
ii. Kuchelewa kuidhinishwa kwa kazi zinazowasilishwa Benki ya Dunia.

### Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kwa kuwa kumekuwa na mapungufu mengi katika utekelezaji wa miradi kama vile gharama kubwa zinatumika ambazo haziakisi uhalisia wa

majengo na miundombinu iliyojengwa. Kamati inaishauri Serikali, kuweka mipango na mikakati thabiti ya kuhakikisha thamani ya fedha inapatikana katika mradi huu.

ii. Kamati imeelezwa kwamba, mradi huu unatekelezwa na taasisi nne chini ya usimamizi wa Afisi ya Rais Fedha na Mipango. Taasisi hizo ni Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ; Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale; Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi; na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi. Kamati inasisitiza umuhimu wa kushirikishwa kwa karibu wanufaika (beneficiaries) ili waweze kutekeleza mradi huu kwa ufanisi.

## MRADI WA UIMARISHAJI WA UTALII KWA WOTE

Mradi wa Uimarishaji wa Utalii kwa Wote ulibuniwa na kuanza kutekelezwa mwaka wa fedha wa 2018/19 kupitia Fungu J02 linalosimamiwa na Katibu Mtendaji wa Kamisheni ya Utalii. Mradi huu unakusudiwa kutekelezwa katika awamu tatu na baadhi ya shughuli za mradi zinakusudiwa kutekelezwa kupitia sekta binafsi au mashirikiano ya pamoja baina ya sekta binafsi na sekta za umma (PPP).

Miongoni mwa madhumuni ya kuanzishwa kwa mradi ni kuwawezesha wananchi kupata soko la bidhaa zao katika sekta ya utalii, kuwawezesha wananchi kushiriki katika sekta ya utalii, kusaidia ujenzi wa jengo la historia la Bikhole kutembelewa na watu wengi zaidi kutoka ndani na nje ya nchi na kuratibu vyema utalii wa bahari.

Awamu ya kwanza ya mradi huu ambayo ilipangwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2018/2019 na 2019/2020, ilipangiwa kutumia jumla ya TZS 2.80 bilioni ambapo fedha zilizopatikana ni TZS 1.55 bilioni ambazo ni sawa na asilimia 55.36 ya kiasi kilichopangwa. Aidha, awamu ya pili ya mradi ilipangwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2020/2021 lakini hakukuwa na fedha

zilizoingizwa mpaka mwaka wa fedha unaisha.

Mradi huu ulipangwa kuendelea kutekelezwa katika mwaka huu wa 2021/2022 kwa kutengewa TZS 2.0 bilioni.

Changamoto za Mradi

i. Kukosekana kwa fedha za kutosha na kwa wakati za kutekeleza mradi kwa mujibu wa mpango wa utekelezaji na mikataba.
ii. Kamati ilipofuatilia utekelezaji wa Mradi huu, ilipewa maelezo juu ya kukosekana kwa fedha za mradi zilizotengwa kwa awamu ya pili ambazo ni TZS2 bilioni kwa mwaka wa fedha wa 2020/2021 na kupelekea Kampuni ya Kin Investment Ltd kutokufanya kazi zilizopangwa katika ujenzi wa jengo la historia la Bikhole ikiwemo ujenzi wa bustani, vyoo, kituo cha mapokezi na ulinzi, maduka ya kutoa huduma za vyakula na vinywaji, kuweka lami, vikalio, kuchimba kisima, usambazaji maji pamoja na uwekaji taa katika eneo.

Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati imebaini kwamba, nguvu yetu ya kuwekeza katika sekta ya utalii ni ndogo sana na haiendani na utegemezi wetu kwa sekta hii. Sisi tuna matumaini makubwa katika kufaidika na utalii lakini uwekezaji wetu bado ni duni. Kamati inaishauri Serikali, kuipa kipaumbele cha kuingizia fedha kama inavyohitajika katika miradi ya sekta ya utalii sambamba na kubuni miradi mikubwa na itakayoleta tija katika sekta hii.
ii. Serikali iimarishe ukusanyaji na utunzaji wa takwimu za wageni wanaotembelea vivutio vya utalii ili ijuwe maeneo ya kuyatilia nguvu zaidi katika usimamizi wake.
iii. Kamati inaishauri Serikali katika kutekeleza miradi ya maendeleo, kuzipatia taasisi husika fedha zinazohitajika kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zilizopangwa. Kutokupatikana kwa fedha za mradi kunazorotesha utekelezaji wa miradi na hatimae kushindwa kukamilika na kuwanufaisha wananchi kwa wakati.

## MRADI WA UHUISHAJI NA UIMARISHAJI WA MFUMO WA USAMBAZAJI MAJI ZANZIBAR (INDIA)

Mradi huu upo katika hatua za awali za utekelezaji na unagharamiwa na Serikali ya India kupitia Mkopo kutoka Benki ya Uagizaji na Usafirishaji ya India (Export – Import Bank of India – "EXIM Bank of India" wenye thamani ya USD 92.18 milioni na mchango wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) ni TZS 600 milioni ambapo fedha zake huingizwa kila mwaka kwa kadri zinavyopatikana. Lengo la mradi ni kuhakikisha upatikanaji endelevu wa maji safi, salama na ya kutosha kwa gharama nafuu kwa watu na sekta zote.

Maeneo yaliyokusudiwa kutekelezwa mradi huu ni maeneo ya Wilaya ya Magahrib "A", Wilaya ya Magharib "B", Wilaya ya Kati, Miji Midogo ya Tunguu na Fumba, Maeneo Huru ya Uwekezaji, Utalii na Viwanda ya Nyamazi.

Kazi kuu zinazotarajiwa kutekelezwa katika mradi huu ni uchimbaji wa visima 64 vyenye uwezo wa kuzalisha lita 792,000 za maji kwa saa, ujenzi wa matangi 14, ulazaji wa mabomba na ufungaji wa mita (House Connections) kwa wateja katika maeneo ya mradi.

### Changamoto zilizopo katika Utekelezaji wa Mradi

i. Mchango wa Serikali katika mradi ni TZS 600 milioni. Katika utekelezaji halisi wa Mradi, Kamati imeelezwa kuwa, fedha zinazoingizwa katika mradi kwa mchango wa Serikali ni kwa mujibu wa fedha zinavyopatikana na haikuainishwa kiwango maalum cha upatikanaji wake.

### Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inashauri kuainishwa kwa kiwango maalum cha fedha za mchango wa Serikali katika utekelezaji wa mradi kwa kila kipindi cha utekelezaji ili iweze kufahamika wazi mchango wa Serikali katika kufanikisha kazi zilizokusudiwa kutekelezwa.

ii. Kamati inashauri Mamlaka kutoa elimu kwa wananchi juu umuhimu wa kutunza miundombinu ya maji inayotarajiwa kujengwa kupitia mradi ili iweze

kutumika na kuwanufaisha wananchi kwa muda mrefu.

iii. Licha ya maeneo ya mradi kuainishwa, Kamati inasisitiza umuhimu wa kuangaliwa mahitaji halisi ya visima kwa maeneo yanayotarajiwa kuchimbwa.
iv. Kwa kuwa mradi unahusisha ufungaji wa mita kwa wateja katika maeneo ya mradi, Kamati inashauri kuangaliwa mapema ubora wa miundombinu wakati wa ufungaji wa mita hizo mpaka kuwafikia wananchi hao.
v. Kamati inaishauri Mamlaka kuangalia vyanzo vya maji vilivyopo katika maeneo ya Mradi vinakidhi kupokewa mabomba yanayotarajiwa kulazwa ili Mamlaka kujiridhisha na uhakika wa miundombinu hiyo katika upokeaji wa maji.

## MRADI WA UCHIMBAJI WA VISIMA ZANZIBAR - RAS EL KHAIMAH

Mradi wa Uchimbaji wa Visima Zanzibar una lengo la kuwafikishia wananchi wa Unguja na Pemba huduma ya maji safi na salama, unatekelezwa kwa USD 1.7 milioni kutoka Mtawala wa Ras el Khaimah. Kwa upande wa Serikali, fedha zinazoingizwa katika mradi huu ni kwa mujibu wa fedha zitakavyopatikana katika bajeti.

### Changamoto zilizopo katika Utekelezaji wa Mradi

i. Kukosekana kwa mkataba kwa ajili ya utekelezaji Mradi umepelekea kutofahamika kwa makubaliano halisi ya uchimbaji wa visima hivyo na namna kazi za uchimbaji visima unavyofanyika, gharama za uendelezaji visima, kukosekana kwa pampu za kutosha zilizohifadhiwa kwa ajili ya kuhudumia visima hivyo pindi pampu zinapoharibika na pia taratibu za ununuzi wa pampu nyengine zinachukuwa muda mrefu.
ii. Baadhi ya visima vilivyochimbwa katika maeneo ya Jumbi Kibondeni, Kidimni Kidarajani na Mwera Pongwe havijawanufaisha wananchi waliopo katika maeneo hayo.
iii. Visima vilivyokamilika katika baadhi ya maeneo kushindwa kufanya kazi

kutokana na gharama za uendeshaji wa visima hivyo kuachiwa Serikali. Kamati ilielezwa kuwa, gharama za kuendesha visima hivyo ni kubwa hasa kwa kuzingatia changamoto ya upatikanaji wa fedha.

Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inashauri juu ya umuhimu wa kushirikishwa wadau wote katika utekelezaji wa miradi tokea hatua za awali ili kubaini mapungufu na changamoto za mradi husika tokea awali na kuweza kufanya maamuzi sahihi katika kutekeleza miradi ya maendeleo.
ii. Kamati inaishauri Mamlaka ya Maji kuwa na timu ya ufundi (Technical Team) katika utekelezaji wa miradi ambayo itasaidia katika usimamizi na kuhakikisha taratibu zote zinafuatwa za mradi.
iii. Kamati inashauri katika miradi ya usambazaji maji ambayo baada ya kukamilika kwake itasimamiwa na jamii inayoziunguka, taasisi husika kufanya makubaliano ya mapema na jamii katika uchangiaji wa gharama za miradi hiyo tokea hatua za awali ili iweze kujiridhisha juu ya utayari wa wananchi katika miradi inayotekelezwa na Serikali pamoja na kuifanya kuwa endelevu.
iv. Kamati inashauri katika maeneo ambayo visima havijawanufaisha wananchi kuchukuliwa jitihada madhubuti ya kuhakikisha kuwa visima hivyo vinaendelezwa pamoja na kugawana gharama za kuvifufua visima hivyo baina ya Serikali, Mkandarasi na Mshauri Elekezi.

## MRADI WA UIMARISHAJI WA MAENEO YA VIWANDA (INDUSTRIAL PARK) - UNGUJA NA PEMBA

Kamati ya Bajeti ilipokea Taarifa ya Mradi wa Uimarishaji wa maeneo ya Viwanda (Industrial Park) ikijumuisha maeneo matatu ambayo ni eneo la Chamanangwe liliopo katika Wilaya ya Wete, Mkoa wa Kaskazini Pemba, eneo la Nungwi liliopo Wilaya ya Kaskazini A Unguja na eneo la Dunga liliopo katika Wilaya ya Kati Unguja. Kamati ilielezwa kuwa maeneo haya yapo katika hatua tofauti za

uwekezaji na ilipata fursa ya kukagua eneo la Dunga Unguja na Chamanangwe Pemba.

Changamoto za Mradi kwa Upande wa Unguja

i. Wizara kupangiwa bajeti ndogo ukilinganisha na kazi ambazo zinatarajiwa kutekelezwa kunarudisha nyuma utekelezaji wa shughuli za mradi.
ii. Kasi ndogo ya upimaji wa maeneo ya mradi kunapelekea kazi nyengine kutoendelea kutokana na kutokuwa na ramani kamili ya eneo linalokusudiwa kutumika kwa shughuli za viwanda.
iii. Wananchi kuvamia maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya shughuli za viwanda hasa wanapobaini kwamba Serikali wanataka kutumia maeneo hayo kwa shughuli za uwekezaji.
iv. Mwitiko mdogo wa wananchi na kuchocheana wenyewe kwa wenyewe katika migomo na kuzuia maeneo hayo kwa uwekezaji.

Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inashauri Serikali kusimamia upimaji wa maeneo yote ya uwekezaji yaliyobakia (Dunga na Nungwi) kwa haraka ili yaweze kutambuliwa , kupatikana kwa mpango wa matumizi wa maeneo hayo na shughuli nyengine ziweze kufanyika.
ii. Kamati inasisitiza Wizara, katika eneo la Dunga kutafuta Mshauri elekezi kwa ajili ya kusaidia kutoa ushauri wa matumizi sahihi ya maeneo hayo.
iii. Kamati inaitaka Serikali kusimamia taasisi husika katika suala la upelekaji wa miundo mbinu mbali mbali katika maeneo ya uimarishaji wa viwanda ikiwemo barabara ili maeneo hayo yaweze kufika kwa wepesi kwani katika eneo la Dunga barabara ya asili ndio inayotumika kufikia eneo hilo.

Changamoto za Mradi kwa Upande wa Pemba

i. Kuwepo kwa mgomo kwa baadhi ya wananchi wa maeneo yaliyofanyiwa tathmini kwa ajili ya kulipwa fidia hali inayoweza kuzorotesha utekelezaji

halisi wa mradi.

ii. Katika tathmini iliyofanyika, kumejitokeza hali ya kujirejea kwa majina na hivyo kuhitajika muda wa kujiridhisha kwa lengo la kuepuka kufanya malipo kwa wasiostahiki.
iii. Kujitokeza kwa watu ambao ni miongoni mwa warithi kutaka kuchukua malipo bila ya ridhaa kutoka kwa warithi wenzao.
iv. Kutokukamilika kwa upembuzi yakinifu na mpango wa matumizi ya ardhi katika eneo la mradi katika kiwango kianachohitajika.
v. Kukosekana kwa majina ya wenye mashamba katika ripoti ya tathmini kutokana na kutofahamika na kutojitokeza kwa wahusika wakati tathmini ikiendelea kufanyika.

Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inashauri katika ulipaji wa fidia kwa wananchi wenye mashamba na vipando, Wizara kuwa makini katika malipo hayo kwa kuwapa wanaostahiki pamoja na kuweka kumbukumbu za malipo vizuri ili ziweze kutumika pindi zitakapohitajika.
ii. Kwa kuwa, kumekuwa na tabia ya wananchi kuvamia maeneo yanayoendelezwa na Serikali kwa shughuli za miradi na kuleta mgogoro katika utekelezaji wa miradi, Kamati inaziagiza taasisi husika kufanya usimamizi madhubuti wa maeneo mbali mbali ili kuepusha migogoro ya ardhi nchini.
iii. Kamati inaishauri Serikali kusimamia maeneo yake pamoja na kuwa na mpango wa muda mrefu wa matumizi ya ardhi kwa maeneo tofauti ili kuepusha uvamizi wa maeneo hayo na ulipaji wa fidia ambao unaigharimu sana Serikali katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.
iv. Katika kuhakikisha matumizi mazuri ya maeneo ya uwekezaji, Kamati inashauri kutambuliwa na kupimwa kwa maeneo mbali mbali ya uwekezaji pamoja na kupatiwa kwa hatimiliki kwa maeneo yote.

## MRADI WA USAFISHAJI WA MAJI TAKA KATIKA ENEO LA MSINGINI CHAKE CHAKE - PEMBA

Kamati ya Bajeti ilipata fursa ya kupokea taarifa ya utekelezaji wa Mradi huu pamoja na kutembelea maeneo ya Mradi husika. Lengo la Mradi ni kusafisha maji machafu yanayotoka katika makazi ya watu kabla ya kuingia katika bahari na kusababisha uchafuzi wa mazingira. Aidha, mradi unalenga kuzidisha kiwango cha ufanisi wa ukusanyaji na usafishaji wa maji machafu yanayozalishwa kutoka kwenye kaya zilizopo katika maeneo ya mji wa Chake Chake, ujenzi wa miundombinu mipya na marekebisho ya mitaro ya zamani na kukarabati muundo wa mfumo wa mitaro kulingana na usawa wa kina cha bahari.

Fedha za Mradi zilizopangwa TZS 686,550,000 mpaka kufikia Septemba 2021 TZS 38,185,871.95.

### Changamoto za Mradi

i. Kamati imebaini uhaba wa uingiaji wa fedha za mradi.
ii. Mitaro ya kuchukulia maji machafu iliyopo maeneo ya Msingini ipo wazi hali inayoweza kupelekea athari kwa jamii inayoizunguka mitaro hiyo.

### Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inaishauri Afsi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kuendelea kutoa elimu kwa jamii juu ya umuhimu wa kutunza miundombinu ya usafirishaji maji machafu ili malengo ya kuwekwa miundombinu hiyo iweze kufikiwa.
ii. Kamati inaishauri jamii kuchukua jitihada za kupambana na athari za mazingira kwa kuepuka shughuli zinazoathiri mazingira yetu.
iii. Kamati inasisitiza usimamizi mzuri wa mimea itakayotolewa katika mabwawa na kukaushwa kwa ajili ya kutumika wakati wa mafunzo ya kazi za mikono kwa jamii.

## PROGRAMU YA KUIMARISHA MIUNDOMBINU YA ELIMU NA MRADI WA KUIMARISHA ELIMU MBADALA NA MAFUNZO YA AMALI

Madhumuni ya Mradi wa Kuimarisha Elimu Mbadala na Mafunzo ya Amali ni kuwajengea vijana uwezo wa kupambana na soko la ajira kwa kuwapatia mafunzo ya Amali na Elimu Mbadala. Kwa mwaka wa 2021/2022, Mradi umepangiwa jumla ya TZS 10,598,8999,000 zikijumuisha TZS 10,065,667,000 za Serikali na TZS 553,232,000 za Washirika wa Maendeleo.

### Changamoto Zilizopo

i. Upatikanaji mdogo wa fedha za Miradi ambapo kwa upande wa Mradi wa kuimarisha Elimu Mbadala na Mafunzo ya Amali, mpaka kufikia Disemba 2021, jumla ya TZS 1,569,334,000 sawa na asilimia 14.8 zimepatikana hali inayokwaza utekelezaji wa miradi kwa muda uliokusudiwa. Aidha, Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Elimu, kati ya fedha zilizopangwa katika mradi huu TZS 60,663,708,000 , mpaka kufikia Disemba 2021 jumla ya TZS 2,249,000,000 zimepatikana sawa na asilimia 3.7.

ii. Kamati imebaini kuwa, utekelezaji wa miradi haufikiwi kwa kiwango kinachostahiki na kwa muda uliokusudiwa kutokana na changamoto ya upatikanaji wa fedha.

iii. Kamati imebaini kuwa, kukosekana kwa usimamizi madhubuti wa miradi katika hatua za awali kunaweza kupelekea miradi kutotekelezwa kwa kiwango kinachostahiki na kwa kipindi kifupi kujitokeza athari mbali mbali.

iv. Fedha zinazotengwa katika bajeti zinazohusisha utekelezaji wa miradi kutoenda sambamba na taarifa zinazowasilishwa katika Kamati wakati wa ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi.

v. Kamati imebaini katika ujenzi wa vituo vya mafunzo ya amali kuchanganywa na utekelezaji wa miradi mengine na ambapo utekelezaji wake ulitakiwa kufanyika peke yake bila ya kuchanganywa na utekelezaji wa miradi mengine.

### Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inashauri katika utekelezaji wa Mradi Kuimarisha Elimu Mbadala na Mafunzo ya Amali unaohusisha ujenzi wa vituo vitano vya amali katika maeneo ya Fumba, Jendele, Pangatupu, Tumbe na Chambani ubakie kama ulivyokusudiwa bila ya kuchanganywa na utekelezaji wa miradi mengine.
ii. Kamati inashauri utekelezaji wa miradi uende sambamba na bajeti zilizotengwa na vigezo vilivyokusudiwa ili malengo ya miradi yafikiwe na kuwanufaisha walengwa.
iii. Kamati inaishauri Wizara kusimamia matumizi sahihi ya fedha zinazopatikana katika utekelezaji wa miradi kwa kuhakikisha kuwa, fedha zinazotumika zinakwenda sambamba na thamani ya miradi inayotekelezwa.
iv. Katika utekelezaji wa Mradi wa Miundombinu ya Elimu, Kamati inashauri kuwepo kwa uwiano wa uendelezaji wa miundombinu ya elimu katika Wilaya kwa kulinganisha na matokeo ya mtihani yanayopatikana ili kuweza kusaidia kwa skuli ambazo miundombinu yao haijitoshelezi.

## MRADI WA UJENZI WA MIUNDOMBINU YA UMWAGILIAJI MAJI ZANZIBAR

Kamati ya Bajeti katika muendelezo wa kazi zake ilipokea taarifa ya Mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya umwagiliaji Zanzibar kwa lengo la kufahamu hatua zilizofikia za utekelezaji wa mradi huo na mambo mengine yanayohusiana na utekelezaji wa mradi.

### Changamoto za Mradi

i. Kupunguzwa kwa eneo la utekelezaji wa mradi kwa upande wa Pemba katika Bonde la Makwararani kutokana na sababu mbali mbali ikiwemo wananchi kutokubaliana na ujenzi wa mradi huo.
ii. Kukosekana kwa fedha za kuwalipa wataalamu wanaosimamia mradi na kupelekea Wizara kutumia fedha za matumizi mengine (other charges) katika kuwalipa wataalamu hao.
iii. Kutokukamilika kwa malipo ya fidia kwa wananchi kwa baadhi ya maeneo ya

Unguja na Pemba.

iv. Kutokubadilishwa kwa gharama za mradi baada ya kupungua kwa utekelezaji wa eneo la mradi kutoka hekta 1524 mpaka hekta 1053.

v. Kutokuwajibika ipasavyo kwa mshauri elekezi wa mradi katika kusimamia kazi hali inayochangia kutogundua kasoro zinazojitokeza kwa wakati katika utekelezaji wa mradi.

vi. Mradi kuhitaji usimamizi wa karibu sana kutokana na mkandarasi kudai malipo ya mradi kwa kukiuka taratibu na Mshauri elekezi kutokuwa makini katika kushauri utekelezaji wa mradi.

vii. Kamati kutoridhishwa na ujenzi wa misingi ya udongo kwa ajili ya kupitishia maji katika Bonde la Mlemele.

Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inaishauri Wizara kuwa makini katika kuangalia utekelezaji wa miradi na gharama zinazotumika hasa katika kipindi ambacho miradi hio hukabiliana na marekebisho mbali mbali.

ii. Kamati inaitaka Wizara kumuwajibisha Mshauri elekezi kwa kutokushauri vyema katika ujenzi wa misingi ya kuptitishia maji katika Bonde la Mlemele.

iii. Kamati inaitaka Wizara kufuatilia na kudhibiti maeneo yake mbali mbali hasa yale ambayo yanatarajiwa kutumika kwa utekelezaji wa shughuli za miradi kwa lengo la kuepusha wananchi kuvamia maeneo hayo na baadae kudai fidia kutoka Serikalini.

iv. Kamati inaishauri Wizara katika hatua mbali mbali za utekelezaji wa miradi kufiuata taratibu zinavyoelekeza za utekelezaji wa miradi hiyo ili malengo yake yaweze kufikiwa kwa ukamilifu na kuleta tija.

## MRADI WA KUJENGA UWEZO NA MATENGENEZO YA MIUNDOMBINU YA UMEME ZANZIBAR (CBMP) NA MRADI WA KUIFANYIA MABADILIKO SEKTA YA NISHATI (ZEST) PAMOJA NA KUFANYA ZIARA KATIKA BAADHI MAENEO YA MIRADI HIYO

Kamati ilipofuatilia utekelezaji wa Mradi wa Kuifanyia Mabadiliko Sekta ya Nishati Zanzibar (ZEST) kwa kipindi cha Julai - Disemba 2020/2021 imebaini kuwa, licha ya mradi huo kutengewa fedha jumla ya TZS 17.85 billioni katika mwaka wa fedha 2020/2021 na TZS 19.2 bilioni katika mwaka wa fedha 2019/2020, utekelezaji wake bado haujaanza kabisa na hakuna uwezekano wa kuweza kutekelezwa katika mwaka huu wa fedha. Mradi huo bado upo katika hatua za maandalizi na bado ratiba ya vikao na Benki ya Dunia kuhusu uidhinishwaji wa fedha za mradi zinaendelea na zinatarajiwa kukamilika Septemba, 2021.

### Changamoto za Shirika katika kutekeleza Miradi hiyo

i. Shirika la Umeme linakabiliwa na changamoto ya kutolipwa madeni ya umeme ya taasisi za Serikali, hali inayoathiri mapato ya Shirika na kuathiri uwezo wa Shirika katika kutekeleza majukumu yake.

ii. Gharama za kuunganisha umeme ni kubwa ukilinganisha na uwezo wa wananchi katika kulipia gharama hiyo.

iii. Mabadiliko ya viwango vya mishahara yaliyopelekea kushuka kwa mishahara ya watumishi wa Shirika la Umeme yametokana na vigezo vilivyotumika kuwapima Shirika pamoja na Mashirika mengine ya Serikali na ambapo vigezo hivyo havina uhalisia kutumika kupima kwa taasisi zote. Kuna haja ya kuupitia upya muongozo wa mishahara na maposho kwa taasisi zote utakaoenda sambamba na kuweka vigezo vinavyoendana na majukumu yanayofanyika kwenye taasisi husika.

Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inaishauri Serikali kuwasaidia wananchi gharama za umeme kwa kufanya punguzo (subsidize) la gharama hizo ili wananchi walio wengi waweze kuzimudu.

ii. Kuna haja kubwa kwa Serikali, kuupitia upya muongozo wa mishahara na maposho kwa taasisi zote za umma utakaoenda sambamba na kuweka vigezo vinavyoendana na majukumu yanayofanyika kwenye taasisi husika.

iii. Kamati inalishauri Shirika la Umeme kuweka utaratibu wa kuwakopesha wananchi wanaotaka kuunga umeme na kuwaruhusu kulipa kidogo kidogo ili kuwapunguzia mzigo wa gharama, hasa ikizingatiwa kuwa wananchi wengi wanahitaji huduma hiyo lakini hali ya kipato chao haiwaruhusu kuweza kutoa fedha zote kwa pamoja.

iv. Kamati inalishauri Shirika katika utekeleaji wa Miradi lizingatie sana suala la uendelevu (Sustanability), Kamati imebaini licha ya kuwa Serikali inatumia fedha nyingi katika miradi, lakini miradi mingi inakosa uendelezaji mzuri.

v. Kamati inalishauri Shirika wakati wa kufanya tathmini ya zabuni za miradi izingatie kuwapa wakandarasi wenye uwezo, ili kuepuka kusimama na kuchelewa kukamilika kwa miradi hiyo wakati Serikali itakapochelewa kufanya malipo.

vi. Shirika limeshauriwa na Kamati litumie teknolojia ya kisasa hususani katika utumiaji wa vifaa, kwakuwa bado Shirika linatumia teknolojia ya kizamani ambayo bila shaka inapunguza ufanisi wa Shirika.

vii. Kuna haja ya kuwa na mawasiliano baina ya Taasisi za Serikali katika Mipango ya Nchi. Mathalan, eneo linalokusudiwa kuwekwa mji kila taasisi ya Serikali ambayo inawajibu wa kuweka miundombinu ishirikishwe ili huduma zote zinazohitajika zipatikane kwa wakati (Mfano Maji, Umeme na Barabara)

viii. Kwakuwa Shirika la Umeme lina madeni mengi inayodai Taasisi za Serikali hususan ZAWA na mbayo kimsingi ZAWA hawawezi kuyalipa, Kamati

inaishauri Serikali kutafuta ufunguzi wa changamoto hii.

ix. Kamati inalishauri Shirika kuendelea na juhudi za kudhibiti wizi wa umeme ambao unaligharimu Shirika upotevu wa takriban TZS 320 milioni kwa mwezi.

x. Kamati inatilia shaka utekelezaji wa Mradi wa Kujenga Uwezo na Matengenezo ya Umeme Zanzibar (CBMP) ambapo ulianza utekelezaji wake 2014 na matarajio ya kumalizika kwake ni 2018. Kutokana na taratibu za manunuzi kukwamisha utekelezaji wa mradi na kupelekea mradi huo kutarajiwa kumalizika 2022. Kuna haja ya kufanyika tathmini ya kina kwa miradi inayotaka kutekelezwa ili kuepusha sababu zitakazokwamisha utekelezaji wa miradi hiyo.

## TAARIFA YA UKODISHWAJI WA VISIWA VIDOGO VIDOGO VILIVYOPO UNGUJA NA PEMBA AMBAVYO VINATUMIKA KWA SHUGHULI ZA UTALII

Kamati ya Bajeti ilikuatana na watendaji wa Kamisheni ya Utalii, Kamisheni ya Ardhi na Mamlaka ya Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) kwa lengo la kupata taarifa ya ukodishwaji wa visiwa vidogo vidogo vilivyopo Unguja na Pemba vinavyotumika kwa shughuli za utalii na kufahamu mapato yanayopatikana kutokana na ukodishwaji huo. Miongoni mwa taarifa iliyopatiwa Kamati ni kuwa, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekodisha jumla ya visiwa 11 vidogo kwa kampuni tofauti kwa lengo la kuendesha miradi ya uwekezaji. Kati ya visiwa hivyo, vipo vilivyokodishwa vyote na vyengine vimekodishwa sehemu ya visiwa hivyo.

### Changamoto zilizopo katika Ukodishwaji wa Visiwa Vidogo Vidogo

i. Muda mkubwa wa ukodishwaji wa visiwa. Kuna baadhi ya visiwa vimekodishwa kwa muda wa miaka 33 ikiwemo kisiwa cha Chumbe, kisiwa cha Mnemba, kisiwa cha Changuu, kisiwa cha Bawe na visiwa vyengine vimekodishwa kwa wawekezaji kwa muda wa miaka 49 kama Kisiwa cha Fundo na Kisiwa cha Shamiani

ii. Gharama za bei ya leseni zinazotozwa na Kamisheni ni ndogo ukilinganisha na aina ya miradi inayoekezwa na rasilimali zilizopo katika visiwa hivyo.
iii. Wawekezaji wengi waliokodishwa katika visiwa hivyo ni wageni ukilinganisha na wazawa.
iv. Kamati haikujabainishiwa utaratibu mzuri iwpo muwekezaji kurudisha kisiwa Serikalini iwapo atakuwa hataki kuendelea na biashara na badala yake kumekuwepo na tabia ya muwekezaji kumkabidhi muwekezaji mwengine kuendelea na mradi husika. Hali hii imejitokeza kwa Kampuni ya Arches Zanzibar Limited iliyokodishwa kisiwa cha Mnemba mwaka 1992, kabla ya kukamilisha muda wake ilikabidhi mradi kwa Kampuni ya Beyond Limited kutoka Afrika ya Kusini mwaka 1996.
v. Kutokuwepo kwa maelewano kwa baadhi ya maeneo baina ya muwekezaji na wananchi hali inayopelekea shughuli za uwekezaji kusitishwa. Changamoto hii imejitokeza katika kisiwa cha Kwale kwa muwekezaji kutokuwa na maelewano mazuri na wananchi wanaotumia eneo hilo kwa shughuli za uvuvi.

Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inashauri taasisi zinazohusika na ukodishwaji wa visiwa kukaa na kupitia upya mikataba ya ukodishwaji wa visiwa kwa kuzingatia muda na viwango na malipo yanaendana na thamani ya rasilimali zilizopo katika visiwa hivyo ili kuona hatua za kuchukuliwa katika kurekebisha hali hiyo.
ii. Kamati inashauri katika mikataba ya ukodishwaji wa visiwa, kuwepo kwa kipengele maalum kitakachomuelekeza Kampuni/muwekezaji kurudisha kisiwa Serikalini pindi atakaposhindwa kuendelea na uwekezaji.
iii. Kamati inaishauri Serikali kuwapa kipaumbele wazawa katika ukodishwaji wa visiwa hivi ili waweze kunufaika na rasilimali zao na mapato kubakia nchini.

## MRADI WA MJI SALAMA UNGUJA NA PEMBA

Mradi wa Mji Salama ulianzishwa na Serikali kwa lengo la kudhibiti vitendo vya uhalifu kwa raia na mali zao katika maeneo ya Mji Mkongwe na maeneo mengine ya Mkoa wa Mjini Magharibi. Awamu ya kwanza ya mradi ilitiwa saini tarehe 20/04/2015 baina ya Serikali na kampuni ya Rom Solution kwa ajili ya kuweka miundombinu ya mradi kwa kipindi cha miaka mitano kilichoishia mwezi Juni, 2020.

Serikali imeingia tena mkataba na kampuni ya Rom Solution kwa awamu ya pili ya mradi ambao umeanza utekelezaji wake mwezi wa Julai 2020/2021 na unatarajia kumalizika Disemba 2022/2023. Mradi umetengewa jumla ya dola za kimarekani 10,655,166 sawa na wastani wa TZS 24,773,260,950.

### Changamoto za Utekelezaji wa Mradi kwa upande wa Unguja

i. Kuwepo kwa mazingira yasiyoridhisha ya kufanyia kazi katika kituo Kikuu cha taarifa (Commanding Centre) kilichopo Maisara - Unguja kama vile uhaba wa maji, ufinyu wa ofisi, usafiri kwa wafanya kazi. Aidha maslahi ya watendaji wa kituo hicho hayaridhishi kutoka na kufanya kazi katika mzingira magumu.

ii. Ukosefu wa wataalamu waliobobea kwenye kuendesha mifumo ya kamera za ulinzi Surveillance System “CCTV”

iii. Kutokuwepo kwa mkataba wa matengenezo ya miundombinu (maintance contract) katika mradi wa awamu ya pili

iv. Kutokuwepo kwa kanuni ya kulinda miundombinu ya mradi kwa lengo la kudhibiti uharibifu wa miundombinu hiyo.

v. Ushirikiano hafifu baina watendaji wa Afisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali Mitaa na Idara Maalum za SMZ juu ya usimamizi wa mradi.

### Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inaishauri Serikali kubadilisha usimamizi na uendeshaji miradi wa

kutoka kwa Afisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali Mitaa na Idara Maalum za SMZ na kwenda kwa Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA Zanzibar (ZICTIA). Hii ni kutokana na uwezo mdogo wa kitaalam na gharama kubwa za uendeshaji wa mradi ni changamoto kubwa kwa upande wa Afisi ya Rais.

ii. Kamati inaishauri Serikali kuongeza mafunzo zaidi kwa watendaji waliochaguliwa kuendesha mradi huo. Aidha ni muhimu kwa Afisi ya Rais kuajiri wataalamu wenye weledi katika fani zinazohusiana na CCTV.

iii. Kamati inaitaka Serikali kuharakisha kumaliza utengenezaji wa kanuni zitakazosaidia katika usimamizi wa miundombinu ya mradi

iv. Kamati inaishauri Afisi ya Rais kujipanga kuondoa kasoro zilizopo katika mradi na kuwashirikisha ipasavyo watendaji wote wanaohusika katika usimamizi wa mradi.

Changamoto za Utekelezaji wa Mradi kwa upande wa Pemba

i. Kutokuwepo kwa wataalamu wa kuendesha mitambo katika vyumba vya kuhifadhia taarifa katika kituo cha Wete, Chake Chake na Mkoani.

ii. Ukosefu wa vyombo vya usafiri vya kufuatilia matukio yaliyonaswa katika kamera kama vile pikipiki, gari nakadhaalika.

iii. Kutojengwa kwa vituo vya kudumu vya kuhifadhia taarifa kwa mujibu wa mkataba na badala yake mitambo hiyo kufungwa katika vyumba vidogo kama vituo vya muda ambavyo vimo katika kambi za Idara Maalum za SMZ.

Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inaitaka Afisi ya Rais kuhakikisha wanapeleka vyombo vya usafiri kwa ajili ya kufuatilia matukio kwa upande wa Pemba ili kurahisisha shughuli mbalimbali zikiwemo za kiofisi na ufuatiliaji wa makosa mbalimbali yanayotendeka.

ii. Kamati inaitaka Afisi ya Rais kupelekea wataalamu wa kuendesha mitambo

kwa upande wa Pemba na kutoa mafunzo mbalimali yanayohusiana na uendeshaji wa mitambo na vifaa ambavyo vimo katika vituo vya kuhifadhia taarifa.

iii. Kamati inaitaka Afisi ya Rais kujenga vituo vya kudumu vya kuhifadhia taarifa (Data Centers) kwa mujibu wa mkataba ambavyo vitakuwa na hadhi na sifa ya kuwekwa mitambo ya kuhifadhia taarifa hizo.

## MRADI WA VIWANDA VYA USHONI WA NGUO NA VIATU KVZ - MTONI

Mradi wa Ujenzi wa Viwanda vya Ushoni wa Nguo na Viatu ulianza kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2018/2019 na ulipangwa kutumia jumla ya TZS 1.405,271,595, hadi kukamilika kwa ujenzi huu jumla ya TZS 1,114,367,500 zimetumika sawa na asilimia 79% ya fedha zilizopangwa. Mradi upo katika hatua za mwisho, kwa kumalizia ufungaji wa baadhi ya mashine, kuweka miundombinu ya umeme na kupaka rangi katika jengo la kiwanda cha ushoni wa viatu ZLSF. Kiwanda cha kitazalisha viatu vya aina mbalimbali vya kiaskari, mikanda ya ngozi, makubazi, mikoba pamoja na vipochi vya ngozi.

Kwa upande wa kiwanda cha ushoni wa nguo, kinalenga kushona sare za wapiganaji wa vikosi vya SMZ pamoja na kushona nguo tofauti za kiraia kama vile sare za skuli, sare za ofisini na mahotelini na nguo nyengine mbalimbali.

Kiwanda kitakapokamilika kwa ufungaji wa mashine zake kitakuwa na uwezo wa kushona nguo 500 kwa siku. Aidha, kwa kipindi cha Aprili - Juni kimeweza kushona jumla ya nguo 720 zenye gharama ya TZS. 16,241,690 na kupata faida ya TZS. 3,172,465.

### Changamoto za Utekelezaji wa Mradi

i. Kukosekana kwa mafunzo kwa wafanyakazi wa viwanda, jambo ambalo linarudisha nyuma ufanisi katika uzalishaji wa viwanda.

ii. Kukosekana mali ghafi na baadhi ya vitendea kazi mathalan mashine kwa ajili ya kuzalisha kwa mfumo wa pamoja (line sectioning) na mashine kwa

ajili ya kutengeneza bidhaa mbalimbali za ngozi kama vile viatu vya maafisa na viatu vya kiraia.

iii. Kuwepo kwa madeni makubwa yenye thamani ya TZS 126,339,106 kwa Idara Maalum za SMZ. Madeni hayo yanatokana na ushoni wa sare za wapinaji kutoka vikosi vya Idara Maalum za SMZ.
iv. Kuchelewa kwa taarifa kamili ya tahmini ya mahitaji ya viwanda kumepelekea kutokamilika kwa mpango wa kukamilisha viwanda hivi.
v. Uhaba wa soko kutokana na wananchi kutokuwa na uelewa juu ya bidhaa zinazozalishwa katika viwanda.
vi. Uhaba wa soko kutokana na viwanda kuwemo ndani ya eneo la kambi, hali inayopelekea wananchi kuwa na hofu ya kwenda kupata huduma viwandani hapo.

Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inaishauri Afisi ya Rais kukamilisha mpango wa mafunzo kwa wafanyakazi wa viwanda hivyo ili kuwaongezea ujuzi katika kazi zao za ushoni.

ii. Kamati inasisitiza kukamilishwa na kufanyiwa kazi kwa haraka tathmini ya mahitaji ya viwanda ambayo itasaidia kukamalisha mfumo mzima wa ufanyaji kazi wa viwanda ili viwanda hivyo viweze kuzalisha bidhaa zenye viwango na ubora wa hali ya juu.

iii. Kamati inaishauri Serikali ihakikishe madeni yake wanayodai Idara Maalum za SMZ kwani madeni hayo yanarejesha nyuma shughuli za uendeshaji wa viwanda hivyo.

iv. Kamati inaiagiza Serikali kusaidia kiwanda hichi kwa kupelekea kazi za ushoni wa nguo katika kiwanda.

# SHIRIKA LA NYUMBA ZANZIBAR

Kamati ya Bajeti ilipokea Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Shirika la Nyumba kwa upande wa Afisi ya Pemba kwa kipindi cha Julai - Disemba 2021/2022 kama ni moja ya jukumu la Kamati la kuhakikisha mipango ya Serikali inatekelezwa kama ilivyopangwa.

Kwa kipindi cha Julai - Disemba 2021, Shirika Pemba ilikadiria kukusanya jumla ya TZS 199,500,000 kutoka vyanzo vyake vya mapato hadi kufika Disemba 2021. Shirika limeweza kukusanya jumla ya TZS 172,914,000 sawa na asimilia 86% ya makadirio

Aidha kwa upande wa matumizi, Shirika Pemba lilikadira kutumia Jumla ya TZS 164,757,075 na hadi kufika Disemba 2021, Shirika limetumia jumla ya TZS 119,012,96.64 sawa na asilimia 72% ya makadirio.

## Changamoto za Shirika la Nyumba Pemba

i. Wamiliki wa nyumba binafsi kutotaka kuchangia gharama za matengenezo zinazofanywa na Shirika.

ii. Baadhi wa wapangaji kukwepa kulipa kodi kwa kisingizio cha hali duni ya maisha na kuhisi kwa vile nyumba hizo ni za Serikali wanapaswa kukaa bila ya kusumbuliwa.

iii. Kamati imebaini kuwa Shirika la Nyumba Pemba halina takwimu sahihi ya thamani ya mali zake.

iv. Ukosefu wa wataalamu katika fani ya ujenzi wakiwemo Wahandisi na Wasanifu wa Majengo hali inayopelekea kutumia wataalamu wa nje katika ujenzi wa majengo yao.

v. Ukosefu wa vitendea kazi kama vile vyombo vya usafiri kwa ajili ya kufuatilia shughuli mbalimbali mathalan ufuatiliaji wa mapato na majukumu mengineyo.

## Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inalishauri Shirika kufikiria zaidi juu ya ujenzi wa nyumba mpya za shirika badala ya kutumia fedha nyingi katika kurekebisha nyumba za zamani ambazo wapangaji wake wanakwepa kulipa kodi.

ii. Kamati inalishauri Shirika kufanya mazungumzo ya mara kwa mara na wateja wake na kuwaelimsha juu ya umuhimu ya kulipa kodi.

iii. Kamati inalishauri Shirika kupitia tena na kutengeneza Mpango Mkakati mpya wa Shirika sambamba na kufanya upya tathmini ya thamani halisi ya mali za Shirika.

iv. Kamati inalishauri Shirika kukiimarisha Kitengo cha Ujenzi na Ushauri Elekezi ili kazi zote za ushauri, kandarasi na usimamizi wa miradi ufanywe na Shirika lenyewe ili kupunguza gharama za miradi.

v. Kamati inalishauri Shirika kwa mamlaka yake kuajiri wataalamu wenye fani za ujenzi pamoja na kununua vitendea kazi vikiwemo vyombo vya usafiri katika kufuatilia shughuli mbalimbali za Shirika.

## Ziara ya Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) Dar es Salaam

Kamati ya Bajeti imefanya ziara katika Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) - Tawi la Dar es Salaam kwa lengo la kujifunza namna Shirika hilo linavyotekeleza majukumu pamoja na kufahamu mafanikio na changamoto mbalimbali zinazolikabili Shirika na namna wanavyozitafutia ufumbuzi. Katika ziara hiyo, Kamati imeongozana na baadhi ya watendaji kutoka Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi pamoja na watendaji wa Shirika la Nyumba la Zanzibar (ZHC).

Kamati ya Bajeti imejifunza mambo mbali mbali katika ziara hiyo ambayo yanaweza kusaidia katika ufanyaji kazi wa Shirika la Nyumba la Zanzibar (ZHC) kama ifuatavyo:

i. Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) linafanya shughuli za ushauri elekezi, upangaji, ukadandarasi wa nyumba na majengo kwa majengo yao, majengo

ya Serikali na yale ya taasisi au mtu binafsi jambo ambalo linasaidia kuongeza mapato ya shirika.

ii. Shirika limejipanga katika kusimamia ulipaji wa kodi kwa wakati, kuweka mifumo mipya ya vitasa vya kielektroniki vinavoweza kujifunga iwapo mpangaji wa nyumba atashindwa kulipa kodi kwa wakati.

iii. Shirika limeweza kufanya tathmini ya mali zake inayoonesha kwamba Shirika limeweza kufikia malengo ya kuongeza thamani ya Shirika kwa asilimia 93.

iv. Shirika limeweza kusimamia milki zake kwa kuweza kujenga majengo ya makaazi na biashara katika mikoa mbalimbali ya Tanzania Bara na kufanya shughuli za usimamizi, ushauri na ujenzi wa majengo ya Serikali na taasisi binafsi.

## MRADI WA MFUKO WA MAENDELEO YA JAMII (TASAF III)

Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) ulianzishwa mwaka 2000 kwa lengo la kupunguza umsikini kwa wananchi. Fedha za utekelezaji, usimamizi na uendeshaji wa shughuli za TASAF Zanzibar zinachangiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mfuko wa maendeleo ya jamii (TASAF). Kwa sasa Mfuko wa maendeleo ya jamii (TASAF) inaendelea awamu ya tatu ya kipindi cha pili ambacho kinalenga kujumuisha kaya zote masikini kwa upande wa Zanzibar ambazo hazikupata nafasi ya kujumuishwa katika (TASAF III) kipindi cha kwanza.

### Changamoto za Utekelezaji wa Mradi wa TASAF Zanzibar

i. Kuwepo kwa malalamiko ya baadhi ya wananchi kutoingizwa katika wanufaika na wengine kutolewa katika mradi wa TASAF hali ya kuwa wanavigezo vya kuwa katika mpango.
ii. Hali ya upatikanaji wa fedha za mchango wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar umekuwa sio wa kuridhisha jambo ambalo linazorotesha shughuli mbalimbali za uendeshaji wa TASAF Zanzibar.

iii. Kutofanyika tathmini ya mara kwa mara juu miradi ya ajira za muda ili kubaini kuwa miradi hii inakua endelevu na inawanufaisha jamii.

iv. Uelewa mdogo wa matumizi ya huduma za kibenki na mtandao kwa walengwa hali inayopelekea kuchelewa kupata ruzuku zao.

Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inaishauri Serikali kujitahidi katika kuendelea kutoa mchango wake wa fedha za TASAF Zanzibar kwa wakati ili shughuli za uendeshaji ziendelee bila ya kuzorota.

ii. Kamati inaishauri Serikali, kutoa elimu zaidi kwa walengwa juu ya kutumia njia za kibenki katika kupata ruzuku zao kwa wakati. Njia hii itasaidia pia usimamizi mzuri wa fedha.

iii. Kamati inaishauri Serikali kufanya tathmini ya mara kwa mara ili kubaini kuwa miradi hii ya ajira za muda kwa Shehia inakuwa endelevu na inanufaisha jamii.

iv. Kamati inaishauri Serikali katika utekelezaji wa miradi ya (TASAF) kuwashirikisha ipasavyo jamii juu ya uibuaji wa miradi mbalimbali ili jamii ipatiwe miradi ambayo itaondoa changamoto zinazowakabili katika maeneo yao.

v. Kamati inaishauri Serikali kuendelea na utaratibu wa kuendeleza kuhakiki kaya masikini kwa kutumia timu ya kitaalamu ambayo imeundwa na TASAF ambayo inashirikiana vizuri na uongozi wa Shehia ili kuzibaini kaya ambazo zina vigezo na kuzitoa kaya ambazo hazina vigezo na si vyenginevo ili kuepeshusha malalamiko ambayo yanajitokeza mara kwa mara.

## Ziara ya Kamati katika Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) - Dar Es Salaam

Kamati ya Bajeti ilifanya ziara Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) - Dar es Salaam ili kupata uelewa wa miradi inayosimamiwa na TASAF katika Mkoa wa Dar es Salaam, na kujifunza namna miradi hiyo inavyowanufaisha kaya masikini. Katika ziara hiyo, Kamati pia ilipata fursa ya kuzungumza na kuona miradi inayotekeleza na wanufaika wa TASAF katika baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Dar es Salaam.

Aidha, Kamati imeweza kujifunza mambo mbali mbali ambayo yanaweza kusaidia katika ufanyaji kazi wa TASAF Zanzibar kama ifuatavyo:

i. Kamati imejifunza kuwa mradi wa TASAF umeweza kuleta mafanikio makubwa katika kuinua hali za kaya masikini kiuchumi hatimae kuweza kupunguza ukali wa maisha.

ii. Kamati imejifunza kwamba walengwa wanaopatiwa ruzuku wameweza kujiwekea akiba na kuweza kuunda vikiundi vya akiba kwa ajili kukopa na kufanya biashara mbalimbali zilizowainua kiuchumi.

iii. Kamati imejifunza juu ya utekelezaji wa mradi wa ajira ya muda ulivyowanufaisha wananchi wa mtaa wa Minazi mirefu. Kamati imejionea jinsi walengwa walivyotekeleza mradi wa vitofali (Perving Blocks), ujenzi wa kizimba cha taka katika Skuli ya Sekondari ya Binti Mussa.

## MRADI WA UJENZI WA SKULI YA SEKONDARI NA UFUNDI JKU – MTONI

Mradi wa Ujenzi wa Skuli ya Sekondari na Ufundi JKU - Mtoni kwa awamu ya kwanza ulianza katika mwaka wa fedha 2017/2018 kwa utekelezaji wa ujenzi wa jengo la ghorofa tatu ambalo kwa sasa limekamilika, na limegharimu jumla ya TZS 2,789,865,233. Awamu ya pili ya utekelezaji wa mradi, ulianza mwaka 2018/2019 kwa ujenzi wa Jengo la Skuli ya Ufundi wa JKU lenye ghorofa mbili kwa gharama ya jumla ya TZS 4,081,879.623 na ujenzi upo katika hatua za mwisho za kumalizika kwake.

Changamoto ya Mradi

i. Miundombinu ya mradi ikiwemo marumaru (tiles) katika baadhi ya vyumba vya madarasa kutowekwa kwa mpangilio mzuri na kupelekea kuharibika katika muda mfupi.

ii. Mchakato wa zabuni kuchukua muda mrefu na kupelekea kuchelewa jambo kukamilika kwa mradi pamoja na kuongezeka gharama za mradi kutokana na kupanda bei za vifaa vya ujenzi.

iii. Uchelewaji wa upatikanaji wa fedha za mradi kutoka Serikalini kunapelekea kukwama kwa shughuli mbalimbali za utekelezaji wa mradi

Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inalipongeza Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar (JKU) kwa kuweza kutekeleza mradi wa Skuli ya Sekondari na Ufundi JKU- Mtoni kwa kutumia mafundi wa vikosi na kuweza kupunguza gharama kubwa za ujenzi.

ii. Kamati inalishauri Jeshi la Kujenga Uchumi katika utekelezaji wa miradi kuzingatia ubora wa majengo sambamba na kuongeza wahandisi wa kikosi na kuwashirikiisha ipasavyo Wakala wa Majengo Zanzibar (ZBA) katika kusimamia miradi.

iii. Kamati inaishauri Serikali kuharakisha mchakato wa zabuni katika miradi ya Serikali kwani kuchelewa kwake kunaleta changamoto kubwa katika utekelezaji wa miradi ya Serikali kwa wakati uliopangwa.

iv. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha fedha zilizotengwa kwa ajili ya miradi zinapatikana kwa wakati kwani miradi mingi ya Serikali huzidi gharama kutokana na kuchelewa kwa upatikanaji wa fedha hizo.

v. Kamati inaishauri Jeshi la Kujenga Uchumi kuandaa mfumo mzuri wa kuwaongeza maslahi walimu wa Skuli ya Sekondari na Ufundi JKU ambao ni raia ili kuwapa ari ya kufanya kazi zao kwa ufanisi na kuweza kuzidisha

ufaulu wa wanafunzi wa Skuli hizo.

## MIRADI YA UJENZI WA MAHANGA NA NYUMBA ZA ASKARI WA JKU NA CHUO CHA MAFUNZO

Mradi wa Ujenzi Mahanga na Nyumba za Askari za JKU na Chuo cha Mafunzo, una lengo la kutekeleza azma ya Serikali ya kuhakikisha wapiganaji wa Idara Maalum za SMZ waliopo Zanzibar wanapatiwa makaazi na majengo mazuri kwa ajili ya kuimarisha utendaji wa kazi zao.

### Changamoto za Miradi

i. Kuchelewa kukamilika kwa miradi hii kutokana na kutoingia fedha kwa wakati uliopangwa.

ii. Kuongezeka kwa muda na gharama za utekelezaji wa miradi.

iii. Kuchelewa kwa michoro kutoka ZBA pamoja na mzunguuko mkubwa wa taratibu za manunuzi kutoka kwa Mamlaka ya Ununuzi.

iv. Kutokuwa na wahandisi kwa Chuo cha Mafunzo kulikopelekea kusuasua kwa utekelezaji wa mradi.

### Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inashauri mradi uhusishe upatikanaji wa samani katika majengo yaliyokamilika.

ii. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha fedha zilizotengwa kwa ajili ya miradi zinapatikana kwa wakati. Aidha, Serikali iondoshe urasimu katika mchakato wa zabuni.

iii. Kamati inatoa ushauri kwa Wakala wa Majengo kuharakisha taratibu za michoro ya majengo wanayoyasimamia ili taratibi nyengine za mradi ziweze kuendelea.

## MRADI WA UJENZI WA JENGO LA STUDIO NA OFISI ZA SHIRIKA LA UTANGAZAJI ZANZIBAR (ZBC) - PEMBA

Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Studio na Ofisi za ZBC Pemba upo katika hatua za mwisho za kukamilika. Mradi huu umeanza utekelezaji wake katika mwaka wa fedha 2018/2019 na ulitarajiwa kukabidhiwa Septemba 2020 kwa mujibu wa mkataba, lakini hadi Kamati ilipotembelea mradi huu tarehe 11/8/2021 bado jengo hilo halijakabidhiwa kwa Serikali.

Gharama za awali zilizotengwa katika mradi huu ni jumla ya TZS 1.5 bilioni. Aidha, gharama za mradi zimeongezeka baada ya kusainiwa nyongeza "Addendum" ya TZS 375.974 milioni sawa na asilimia 21 ya gharama ya mradi wote. Hadi kamati ilipotembelea mradi huo mkandarasi tayari ameshalipwa TZS 1,147,696,900.31 sawa na asilimia 64 ya malipo yote. Mkandarasi wa mradi huo ni Chuo cha Mafunzo.

### Changamoto za Utekelezaji wa Mradi

i. Kuchelewa kumalizika kwa mradi, mradi ulitarajiwa kukabidhiwa Septemba 2020 hadi mwaka wa fedha 2021/ 2022 mradi huu bado ulikuwa haujakabidhiwa kwa Serikali.

ii. Ufinyu wa nafasi katika jengo la Studio, kuwepo kwa vyumba vidogo, kutokuwa na mpangilio mzuri wa vyumba na vyoo jambo ambalo limepoteza hadhi jengo hilo.

iii. Kuongezeka kwa gharama za mradi kwa kusainiwa ''addendum'' ambayo ni zaidi ya asilimia 15 ya fedha za mradi ambazo ndio zinaruhusika kisheria.

iv. Uwezo mdogo wa kifedha wa mkandarasi kumepelekea kutokukamilika kwa asilimia iliyobaki ya ujenzi wa jingo hilo.

v. Mradi kutokuwa na usimamizi mzuri na kukiukwa kwa Sheria mbalimbali kama vile kutowashirikisha Wakala wa Majengo Zanzibar (ZBA) na kutokuwa na timu ya kitaalamu ya Wizara ambayo inapaswa kufuatilia kila hatua ya

ujenzi wa mradi huo.

Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati haikuridhishwa na utekelezaji wa mradi kutokana na kukosekana kwa thamani halisi fedha zilizotumika ukilinganisha na jengo lenyewe. Aidha, jengo hilo linaonekana kutokidhi shughuli za studio kutokana na ufinyu wa nafasi. Kamati inaishauri Serikali kufuata taratibu za kisheria kama vile kuwashirikisha Wakala wa Majengo Zanzibar (ZBA) na kuhakikisha kupatikana kwa thamani halisi ya fedha zilizotumika.

ii. Kamati haikuridhishwa na taratibu zilizotumiwa katika kufanya "addendum" hiyo kwani zimekiuka sheria ya manunuzi ambayo imeweka wazi kuwa "addendum" isizidi asilimia 15 ya fedha zote za mradi na endapo ikizidi basi taratibu mpya za kutangaza zabuni zifanywe jambo ambalo kwa mradi huu halijafanyika. Hivyo Kamati, inatoa msisitizo kwa taasisi za Serikali kufuata Sheria ya manunuzi wakati wa kutekeleza miradi.

iii. Kamati inaishauri Serikali, kutoa fedha za miradi kwa wakati ili miradi hiyo iweze kukamilika katika muda uliopangwa na kuweza kudhibiti gharama za mradi ambazo zinatokana na kupanda kwa bei za vifaa kila mradi unapoendelea kuchukua muda mrefu kukamilika kwake.

iv. Kamati inaishauri Serikali kuwa na usimamizi mzuri wa miradi kwa kuunda timu za kitaalamu za Wizara kwa mujibu wa Sheria ya Manunuzi ambazo zitasaidia katika usimamizi wa hatua mbali mbali za usimamizi wa miradi.

## MRADI WA UJENZI WA BOHARI YA DAWA VITONGOJI - PEMBA

Mradi wa Ujenzi wa Bohari unalenga kuondoa changamoto ya kusafirisha dawa kwa meli kutoka Bohari kuu Unguja kwenda Pemba jambo ambalo lilikuwa linasababisha kutokupatikana dawa kwa wakati. Mradi huu unatekelezwa kwa awamu mbili, awamu ya kwanza ya mradi unajumuisha ujenzi wa ghala kuu la kuhifadhia dawa, vifaa vya utibabu, ofisi za wafanyakazi wa bohari, miundombinu

ya uhifadhi, vyumba viwili vya kuhifadhia dawa baridi, jenereta, upelekaji umeme, ujenzi wa barabara na ununuzi wa samani za ofisi. Awamu ya pili ya mradi imejumuisha ujenzi wa uzio (fencing), land scaping, uwekaji wa mfumo wa kuzimia moto, ununuzi wa "forklift" mbili na "pallet jacks".

Kwa awamu ya kwanza mradi umetekelezwa na Kampuni ya Multistruct Building Contractors ya Dar es Salaam kwa gharama ya TZS 1,877,439,629, kati ya hizo fedha TZS 553,495,966 sawa na asilimia 29 ni kutoka Mfuko wa Dunia (Global Fund) na TZS 1,323,943,663 sawa na asilimia 71 kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Awamu ya pili ya mradi umetekelezwa na kampuni ya ZECCON LIMITED kwa gharama ya TZS 597,635,771, mradi ulianza mwenzi Disemba 2020 na unatarajia kumalizika mwenzi Juni 2021.

Changamoto ya Utekelezaji wa Mradi

i. Kuchelewa kumalizika kwa mradi kutokana na sababu mbalimbali za kiufundi na kiutekelezaji zikiwemo mripuko wa maradhi ya UVIKO 19.

ii. Bohari inakabiliwa na upungufu wa wafanyakazi kwani bohari kwa sasa inaendelea na na huduma za uhifadhi na usambazi dawa na vifaa tiba katika hospitali za Pemba.

iii. Gharama za umeme kwa uendeshaji wa bohari ni kubwa ambazo zinafikiaTZS 7,000,000 kwa mwezi.

iv. Kukosekana walinzi wa Bohari kwani waliyokuwepo awali walikuwa ni walinzi wa kampuni ya ujenzi.

Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati imeridhishwa na utekelezaji mradi na kuishauri Serikali kutatua changamoto ndogo ndogo zilizopo katika Bohari iweze nradi huu ulete tija kwa wananchi wa kisiwa cha Pemba.

ii. Kamati inaishauri Serikali, kuongeza wafanyakazi katika bohari ili huduma

za uhifadhi na usambazi wa dawa na vifaa tiba ufanyike kwa ufanisi.

iii. Kamati inaendelea kusisitiza Serikali kupeleka walinzi wa kudumu katika bohari kwa lengo la kudhibiti wizi wa vifaa pamoja na kuimarisha ulinzi katika maeneo ya bohari hiyo.

iv. Kamati inaishauri Serikali kutafuta namna bora ya ulipaji gharama za umeme katika bohari ya kuhifadhia dawa Pemba, kwani kuendelea kuachiwa bohari kulipa deni hilo lipaipa mzigo mzito Wizara ya Afya na linakwamisha utekelezaji wa shughuli nyengine za kiofisi.

## MRADI WA UNUNUZI WA MITAMBO YA UCHAPAJI YA WAKALA WA SERIKALI WA UCHAPAJI ZANZIBAR

Katika kuleta mafaniko ya kiutendaji na ufanisi katika utoaji wa huduma za uchapaji, Serikali imeamua koboresha huduma za Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar kwa kutekeleza Mradi wa Ununuzi wa Mitambo ya Kisasa ya Uchapaji ili kutatua changamoto ya kughushi nyaraka za Serikali, kupunguza malalamiko ya ucheleweshaji wa kazi za uchapaji wa wakala na kuchapisha kazi zenye ubora ili kuleta ushindani katika soko la ndani na nje ya Zanzibar. Mradi umeidhinishiwa jumla ya TZS 9,520,000 na hatua iliyofikia kwa sasa Wakala imeshakamilisha taratibu za zabuni na inasubiri muongozo kutoka Mamlaka ya Ununuzi ili iendelee na hatua nyengiune.

### Changamoto za Utekelezaji wa Mradi

i. Kamati inatia shaka juu ukamilishaji wa mradi huu kwa muda uliokusudiwa kwani mradi umeidhinishiwa fedha katika mwaka wa fedha 2021/2022 na hadi Kamati ipokea taarifa ya mradi huu Januari 2022 Wakala bado walikuwa wanasubiri muongozo wa kufanya manunuzi kutoka Mamlaka ya Ununuzi ilhali imebakia muda miezi michache kabla ya kumalizika kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

ii. Kukosekana kwa taarifa kwa wasambazi wa mitambo wa nchi za nje hususan taarifa za kifedha kutokana na kudhibiti usiri wa taarifa zao.

iii. Kutofautiana kwa taratibu za manunuzi baina ya Zanzibar na nchi wanazotoka wasambazaji, hali ambayo inapelekea kuwepo ugumu wa kuwapata wasambazaji watakaokubali kufuata Sheria ya Zanzibar.

Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inaagiza kuharakishwa kwa taratibu za manunuzi na Mamlaka ya Manunuzi ili mitambo hiyo iweze kununuliwa kabla ya kumalizika kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

ii. Kamati inasisitiza Wakala kuendelea kuwapa mafunzo maalum watendaji wake kuhusu uendeshaji wa mitambo ya uchapaji inayotarajiwa kununuliwa.

## MRADI WA UIMARISHAJI NA UTOAJI WA MATANGAZO YA ZBC

Kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC) limekadiria kutumia jumla ya TZS 19,201,500,000 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vipya kwa lengo kuimarisha huduma za matangazo. Vifaa hivyo ni ununuzi wa gari mbili za kurushia matangazo (OB VAN), ununuzi na ufungaji wa vifaa vya studio ya Unguja na Pemba, ununuzi wa ‘’satellite uplink earth station and fly way’’, ununuzi wa ‘’playout server’’ na softwares za habari, ununuzi wa ‘Live U 6 na Server zake, ununuzi wa vifaa vya OB vya redio na ununuzi wa gari za ZBC.

Katika kutekeleza mradi huu, Shirika limekamilisha taratibu za zabuni na kuziwasilisha ripoti zake kwa Mamlaka ya Ununuzi kwa ajili ya kujiridhisha na taratibui za zabuni zilizofanya na Shirika. Kamati imearifiwa kwamba, Mamlaka ya Ununuzi ilibaini kuwepo kwa changamoto kadhaa katika mchakato wa zabuni uliofanywa na Shirika na iliamua mchakato huo ufanyike upya kwa kufuatwa kwa ukamilifu taratibu za Kisheria ili kuepusha Serikali kupata hasara.

Changamoto za Utekelezaji wa Mradi

i. Kuchelewa utekelezaji wa mradi kulikotokana na kukwama kwa taratibu za manunuzi.

ii. Kuvunjwa kwa Bodi ya Zabuni ya Shirika jambo ambalo linachelewesha kurudiwa kwa mchakato wa zabuni.

iii. Mgongano wa utaalamu baina ya watendaji, Shirika na Bodi ya Shirika pamoja Mamlaka ya Manunuzi jambo ambalo linakwamishwa ukamilishaji wa zabuni.

Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inaishauri Serikali kuwakutanisha Shirika, Wizara ya Habari na Mamlaka ya Manunuzi na kuzitafutia ufumbuzi changamoto zilizopo ili mchakato wa ununuzi wa vifaa hivyo uweze kufanyika ndani ya kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 kilichobaki.

ii. Kamati inaishauri Wizara kuharakishwa uundwaji wa Bodi ya Zabuni ya Shirika haraka iwezekanavyo ili mchakato wa zabuni wa vifaa hivyo uanze kwa haraka na kwa kufuata taratibu za Sheria ya Manunuzi.

## PROGRAMU YA MAENDELEO YA MAKAAZI KWA KIPINDI CHA JULAI - SEPTEMBA 2021/2022

Kamati ya Bajeti katika kutekeleza majukumu yake imefanya kikao na Wizara ya ardhi na maendeleo ya makaazi kwa ajili ya kupata taarifa ya utekelezaji wa Programu ya maendeleo ya makaazi kwa kipindi cha Julai- Septemba 2021, Programu ya Maendeleo ya Makaazi ina jukumu la kuimarisha Makaazi bora na Salama, kuanzisha miji ya kisasa pamoja na kudhibiti shughuli za ujenzi nchini.

Programu hii inasimamiwa na Wakala wa Majengo Zanzibar (ZBA), Shirika la Nyumba la Zanzibar (ZHC), Bodi ya Kondominio, Bodi ya Kudhibiti Kodi za nyumba, Bodi ya Usajili wa Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo na Bodi

ya Usajili wa Wakandarasi.

Changamoto za Utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Makaazi kwa Kipindi cha Julai-Septemba 2021/2022

i. Ukusanyaji mdogo wa mapato kwa Wakala wa Majengo Zanzibar ZBA unaotokana na baadhi ya taasisi za Serikali kutolipa madeni wanayodaiwa na Wakala
ii. Wakala wa Majengo (ZBA) inakabiliwa na uhaba wa wataalamu katika fani mbalimbali za uhandisi, wasanifu, wakadiriaji wa majengo na fani nyenginezo, jambo ambalo linapelekea kusuasua kwa kazi za Wakala
iii. Uhaba wa fedha za matumizi mengineyo (OC) unawapa changamoto Bodi ya Kondominio, Bodi ya Kudhibiti Kodi za nyumba, Bodi ya Usajili wa Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo na Bodi ya Usajili wa Wakandarasi katika kutekeleza majukumu waliyoyapanga.

Maoni na Ushauri wa Kamati

i. Kamati inaitaka ZBA iwajibike ipasavyo katika ukusanyaji wake wa mapato kwani wana vyanzo muhimu vya kukusanya mapato lakini makusanyo yao hayaridhishi hata kidogo.
ii. Kamati inaishauri Wizara kutoa nafasi za ajira kwa vijana wapya wenye sifa zinahitajika ili kuipa nguvu ZBA na kuweza kufanya kazi zake kwa ufanisi mkubwa.
iii. Kamati inaishauri Serikali kutoa fedha za OC za Bodi kama vile zilivyopitisha katika bajeti zao ili Bodi hizi ziweze kutekeleza majukumu waliojipangia.

# SEHEMU YA SABA

## HITIMISHO

Naomba nihitimishe kwa kukushukuru na kukupongeza wewe Mheshimiwa Spika Zubeir Ali Maulid kwa kuliendesha Baraza hili la Wawakilishi kwa weledi mkubwa. Pia nampongeza Mheshimiwa Mgeni Hassan Juma, Naibu Spika kwa kutekeleza vyema majukumu yake ya kukusaidia wewe Mheshimiwa Spika. Aidha, napenda kumshukuru Mheshimiwa Jamal Kassim Ali Waziri Nchi Afisi ya Rais Fedha na Mipango, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Afisi ya Rais Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao waliyoipatia Kamati katika vipindi vyote vya mzunguko wa kazi za Kamati. Nawashukuru pia Mawaziri, Makatibu Wakuu na watendaji wote wa Wizara na taasisi nyengine zilizofanya kazi na Kamati kwa mashirikiano yao mazuri na hatimae kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Kwa namna ya kipekee napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa umahiri, umakini na ushirikiano wao walionipatia wakati wote wa kutekeleza shughuli za Kamati. Aidha, nawapongeza kwa michango yao, maoni na ushauri ambayo imesaidia katika kuhakikisha kuwa Kamati inaisimamia vyema Serikali.

Mwisho kabisa, napenda kuwashukuru watendaji wa Baraza la Wawakilishi wakiongozwa na Katibu wa Baraza Bi. Raya Issa Msellem, kwa ushirikiano wao katika kufanikisha shughuli za Kamati.

Naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu sasa lipokee na kujadili ripoti hii ili hatimae Serikali iende kuyafanyia kazi maoni na ushauri wa Baraza kwa ujumla.

Naomba kutoa hoja.

……………………………….

Mhe. Ali Suleiman Ameir,
Mwenyekiti,
Kamati ya Bajeti,
Baraza la Wawakilishi,
Zanzibar.